# *Kesi Ya Mahakamani*

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya hii, fursa nyingine tuliyo nayo kuja kuzungumza habari za mpendwa Bwana Yesu.

Na sasa, wakati ikiwa inanyesha huko nje, Roho wa Bwana na atunyeshee, ndani, chini mioyoni mwetu, na kutujulisha fadhili Zake za Kiungu, ninii yetu...mapenzi ya Mungu yatakayodhamiriwa maishani mwetu.

Tumeitenga siku hii, Baba, baada ya ibada za asubuhi, na kadhalika, tunaenda kuwaombea wototo Wako wagonjwa. Ninaomba, Mungu, kwamba hii itakuwa ni siku tutakayoikumbuka kwa muda mrefu kwa sababu ya baraka Zako juu yetu.

Tunaliombea kundi hili la wahudumu, ndugu wote, wahudumu wote kote humu nchini. Mungu na azibariki huduma zao na waendelee kukua katika kilindi cha ujuzi wakati wote katika Kristo. Hiyo ndiyo shauku yetu, Bwana, kukujua vizuri zaidi. Ninaombea kila kanisa na kila dhehebu, kwamba litakua katika neema na nguvu za Mungu.

Tunawaombea wagonjwa wote na wanaoteseka, sasa, kwamba wataponywa.

Na kama kungekuwako na nafasi, kuna wengine hapa pamoja nasi, leo hii, wasiokujua Wewe kama Mwokozi wao, jalia hii iwe ndiyo siku ambayo watasema hiyo "Ndiyo!" kwa jumla Kwako.

Libariki Neno Lako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

Hakika ninataka kushukuru, kwanza, kundi hili la wahudumu hapa la—la huu Birmingham, na sehemu za nchi hapa, ambapo wamekuja kwenye udhamini huu, kunisaidia kuja hapa. Nami na—nawaambia, nafikiri wahudumu kama hao wanapaswa kuheshimiwa.

Ninyi, kusanyiko, mnapaswa kumheshimu mchungaji we—wenu, kwa kuwa, mnaona, yeye yuko nje, yeye ni mchungaji. Na akipata kitu ambacho anafikiri kitakuwa lishe bora, ataliongoza kundi lake kwa hicho. Na wakati mwingine, hawakubaliani; wakati mwingine, ni, wengine wao hawakioni hivyo, na labda hawakitaki hicho kwa ajili ya kondoo wao, hawapendi uchungaji wa aina hiyo. Bali nikiwa ni mmoja wa walishaji, pia, mchungaji, ninajaribu tu kuleta Nyasi halisi ya Mungu, Chakula halisi, Neno.

Na kwa hiyo, na—nawathamini sana nami ninaomba ya kwamba Mungu atawabariki daima. Na hebu maisha yao yawe na ushawishi kwa yeyote watakayekutana naye.

Kila mmoja wetu ana huduma. Huduma fulani italivutia jicho la mtu fulani ambapo mwingine hatavutiwa. Mnaona? Kwa hiyo, tunajiweka pamoja, kama nilivyosema hapo mwanzo, kujaribu kuleta yaliyo bora sana tujuayo kwa huduma yetu, huduma yangu, zao, na kadhalika, tunaziweka pamoja kujaribu kuwasaidia enyi watu kujua zaidi juu ya Yesu Kristo, na kuwa bora, watumishi Wake wastahilifu wa—wakati majira yakikaribia ambapo itatubidi kukutana Naye.

Sasa, nataka kuwashukuru wa—watu hapa walioturuhusu kupata kiwanda hiki cha silaha. Hili ni jengo zuri. Nasi tunalithamini hilo sana. Tunawashukuru kwa moyo wetu wote. Nami ninaomba ya kwamba kila mmoja wao, endapo hawajaokoka, wataokoka; na kwenye ule ukumbi mkuu wa Mungu, huko ng'ambo, wakati malaika wakiimba, wakati waliokombolewa wakiingia, mbona, ninatumaini ya kwamba kila mmoja wao atakuwako pasipo kukosekana hata mmoja.

Na sasa, ninawashukuru ninyi watu. Kamwe sikupata nafasi ya kumwuliza meneja, bali ninaamini ya kwamba gharama zote na kadhalika zililipiwa. Nami na—nathamini hilo, kila toleo, kila kitu mlichofanya. Na kwa kawaida wanatoa sa—sada-. . . (Je! walifanya hivyo?) Haikuwabidi kufanya hivyo. Walisema . . . Alisema walitoa sadaka baada ya kila kitu kulipiwa.

Mwajua, nimekuwa me-. . .nyuma ya mimbara, sasa, kwa muda wa miaka thelathini na mitatu. Nami kamwe sijachukua sadaka maishani mwangu, si hata wakati mmoja, hata katika kanisa langu mwenyewe, kamwe sijawahi kuchukua sadaka maishani mwangu. Nilifanya kazi wakati nilipokuwa mchungaji wa kanisa kule, maskani kule Jeffersonville, mimi. . .miaka kumi na saba nikiwa kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma, wala hata wakati mmoja sikuchukua sadaka maishani mwangu. Nililipia matumizi yangu mwenyewe na kadhalika, na kutoa zaka zangu, na kila kitu nilichoweza, moja kwa moja kanisani, na kila kitu kilienda moja kwa moja kanisani.

Na sasa, kwa kawaida huku nje, wao hunipa sadaka. Nami ninataka kulielezea wazi (maana baadhi ya wadhamini wameketi hapa, wapo, sasa): Sadaka ninazopewa, hizo pesa, haziendi moja kwa moja kwangu. Ninapata mshahara kutoka kwa kanisa: ninapata dola mia moja kwa juma, hiyo ni dola elfu tano mia mbili kwa mwaka, dola mia moja kwa juma. Lakini sasa kwa sadaka mnazonipa, zimeteuliwa kwa ajili ya kazi ya Bwana. Hivyo ndivyo wadhamini wanavyofanya nazo: Haziwezi kutumika kwa kitu kingine chochote. Zimetengwa, kama tusemavyo, hata haziwezi kutumiwa kwa jambo lingine lolote. Pesa hizo huingizwa kwenye hazina fulani; ndipo hiyo

hazina ikipanuka, inayoitwa, "kwa ajili ya misheni za nchi za ng'ambo," imetengwa kwa ajili hiyo . . .

Na sasa mara nyingi, nchi za ng'ambo, mnaweza kuona kile tunachokabiliana nacho hapa Marekani, nanyi mwaweza kuwazia jinsi ingekuwa huko. Nasi tunapokwenda huko kwa watu hao maskini wasio na kitu, hata hawana chakula cha kutosha, huko ndani kabisa katika nchi hizo za kipagani . . . Nimewaona maskini mama wamelala barabarani pamoja na watoto wao wachanga, mashavu yao yameingia ndani, na wanakufa, naye mama anajaribu kukupa mtoto huyo; na kama ukimchukua huyo, huyu hapa mwingine, huyu hapa mwingine, mwingine; na hakuna chochote cha kula. Nasi tunatupa kwenye mapipa yetu ya takataka cha kutosha kuwalisha watu hao. Hiyo ni kweli. Hatutambui jinsi tulivyo matajiri.

Na katika misitu ya Afrika na kadhalika, hao watu wana nini cha kunipeleka kule? Hawana hata senti moja, hawana, hawana kabisa njia ya kunipeleka kule. Nami ninajisikia ya kwamba wanapaswa kuisikia Injili, pia, na Injili ambayo—ambayo Bwana Yesu ametupa juma hili.

Ninachukua pesa hizo, maana mimi . . . mnanipa mimi, nami ni wakili wake. Kwa hiyo zinaingia, mimi nikifanya kazi katika wakfu huu, basi haziwezi kutumiwa kwa jambo lingine lolote, ila misheni za nchi za ng'ambo.

Nazo zinaipeleka Injili ii hii moja kwa moja kule kwao. Msininii . . . Ninaenda mwenyewe, kusudi nihakikishe ya kwamba nitafanya vema niwezavyo, nikijua ya kwamba sina budi kuwajibika kwa kila senti ya pesa hizo. Nami ni—ninataka kuwa wakili mzuri kwa Mungu. Na nikiwa siwezi kuwa mwaminifu juu ya mambo hayo, basi nitakuwa mwaminifu vipi juu ya mambo mengine. Mnaona? Kwa hiyo, nataka ku—nataka kuwashukuru.

Basi matoleo niliyopewa (kama—kama vile ndugu ndio kwanza aseme) alasiri ya leo, ni—niliwaomba wasifanye hivyo. Lakini, kwa kawaida kama hawaninii . . . nao wanajua jambo hili: kama matumizi hayawezi kulipiwa, basi tunachukua baadhi ya matoleo hayo, ambayo yametumwa kwa barua, kanisani (ambamo yameteuliwa kwa jambo hili *lingine*), ndipo tunalipia deni ya matumizi. Hatutaki—hatutaki imgharimu mtu yeyote. Mnaona? Kamwe hatuninii . . .

Na kabisa nimemwambia meneja katika kila mkutano (Ndugu Jack Moore, anayeketi hapa, alikuwa mmoja wa watu wangu wa kwanza hudumani; anajua ya kwamba nisingeweza kuvumilia kuombaomba pesa: "Ni nani atakayetoa kiasi *hiki*? Na ni nani atakayetoa *kile*?"), "Pitisheni mfuko wa sadaka, na msahau hilo." Mungu, ni wakati Yeye—wakati atakapoacha kuninii . . . atakapoacha kukimu mahitaji yangu huku nje, ni wakati wangu wa kuondoka hudumani basi. Kwa hiyo, siamini

katika huku kuombaomba, na kuvuta, na kushawishi, na kutisha, na—na chochote kile kwa ajili ya pesa. La, bwana.

Wakati nilipoingia hudumani kwa mara ya kwanza, nilitambua, kote katika historia, kuna mambo matatu yanayomwathiri mtu, mtumishi wa Kristo. Na wakati yeye... Mungu akimbariki na kumpa huduma ndogo, ndipo muda si muda wajua, moja ya maanguko ni *pesa*.

Unaofuata ni *umaarufu*: Wakati anapoanza kuwazia yeye ni *nanii*, papo hapo anaelekea kuanguka. Mnaona. Sisi... hakuna bwana wakubwa miongoni mwetu, sisi sote ni sawa, sisi ni watoto wa Mungu (Mnaona?); hakuna mmoja wetu aliye mkubwa, wala hakuna mmoja wetu aliye mdogo, sisi sote ni watoto wa Mungu.

Basi (pesa, umaarufu), na *wanawake*: Nami ninajulikana kama mchukia wanawake kwa hiyo, mwajua, ninyi, hivyo sivyo kabisa, kwa hiyo hilo—hilo haliko kabisa. Nina mwanamke mmoja, ndiye mwanamke wa pekee ulimwenguni, na huyo ni mke wangu, mwanamke mzuri kuliko wote ambaye Mungu alipata kumweka duniani, kwa ajili yangu. Hiyo ni kweli. Yeye ni wangu, na wangu pekee; nami ni wake, na wake pekee. Na hiyo: nilipokuwa kijana mwanamume niliwazia hilo; sasa ni mzee na ningali ninaliwazia.

Kwa hiyo mimi... yeye... Nimejaribu kuepukana na mambo hayo, na kumwambia Bwana Yesu, "Mungu, ni vigumu sana kuwa huku nje, maana huduma ni tofauti sana. Ina—inawatatiza tu watu kwa kila njia. Nimepitia magumu ya kutosha kupigania vitu *hivyo* na Shetani, sembuse *hawa* wengine." Kwa hiyo, niko tayari kufanya vizuri niwezavyo, kwa ajili ya kila mtu niwezaye; Ufalme wa Mungu utukuzwe.

Sasa, asanteni sana. Nami ninatumaini, siku moja, ninaweza kurudi na kuwaona tena, mnaona, ninatumaini ninaweza.

Pia natumaini wakati nitakapokuja tena... [Kusanyiko lilisema, "Amina."—Mh.] Asanteni. Pia natumaini, nitakapokuja tena, haitakuwa hivi: ambapo una siku tatu; wasiwasi, fadhaa; unaingia haraka, unatoa kitu ambacho, hata hujui unakoelekea; u—u—unashangaa. Ni ajabu mna imani kwake kadiri mliyo nayo. Kama tungaliweza kuketi chini na kuanzia hapa nyuma kwenye Mwanzo, siku baada ya siku, na usiku baada ya usiku, na kuliweka hilo kule chini. Mnaona, kwa namna fulani, mwajua, kidogo unajisikia kama kwamba umezungukwa na mizuka. Mnajua ninalomaanisha. Ha—hamjui.

Kama vile wanafunzi usiku mmoja: Walikuwa huko kwenye bahari yenye dhoruba, na—na maskini mashua ikajaa maji, na—na matumaini yote ya kunusurika yameisha. Nao walikuwa wakipiga makelele, wakilia; hakika, kama Wakristo, walikuwa wakiomba. Mara ghafula wakamwona akija akitembea juu ya maji. Nao wakawazia ilikuwa ni p-... zimwi, walidhani

ilikuwa ni pepo, nao wakaogopa, wakaanza—wakaanza kupiga makelele.

Basi wazieni tu: kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, kilionekana cha kimizuka kwao. Walikiogopa. Hilo limejirudia tena: Wakati tumaini pekee tulilo nalo ni Yeye, pamoja na ahadi Yake hasa ya Neno, na hata hivyo, tunaiogopa (Mnaona?), ku—kuogopa tu kuitumaini. Ni—ni vibaya sana. Lakini kumbukeni, historia daima hujirudia. Haina budi kudumu hivyo. Nami nimewasikia kote katika juma hili, na katika lile lingine . . .

Ninawaona, wengi wenu, labda, huzichukua kanda, na kadhalika, ambazo huduma yangu, kwa njia hiyo, huzunguka na kuzunguka ulimwenguni, kila mahali. Mara nyingi mnanisikia nikisema, "Hayo madhehebu . . ." na kidogo kuyahukumu madhehebu.

Si kwamba ninawahukumu watu; ninahukumu mfumo (Mnaona?); sio dhehebu, watu mle ndani. Loo, la. Watu wangu, hapo awali, walikuwa Wakatoliki; mimi ni wa ukoo wa Kiairishi, hao ni Wakatoliki; nami ninajua kuna Wakatoliki wazuri. Baadhi yao ni watu wangu mwenyewe. Hao ni wazuri. Kuna Methodisti wazuri, Baptisti, Presbiteri, Lutheri; kila dhehebu lina watu wazuri.

Bali mifumo hiyo inayotutenganisha, hicho ndicho kitu ninachopinga. Sisi ni kitu kimoja moyoni. Inatubidi kuwa hivyo. Halafu mifumo yetu, mnaona, huchora mstari wa kimafundisho na huo ndio . . .

Kama kanisa la kwanza liliwahi kuanza, kanisa la kwanza, kanisa lolote, lingesema, "Tunaamini hili," na kulimalizia fundisho lao kwa koma, badala ya nukta, tungeninii . . . kamwe kusingekuwako na kitu ila kanisa moja. Hivyo tu. Mnaona. "Tu—tunaamini jambo hili, pamoja na kiasi kile Mungu atakachotujalia kujua vinginevyo." Lakini tunaposema, "Tunaamini jambo *hili*, na *hili* ndilo, na *lile* pekee": basi, tunakufa papo hapo, mnaona, kwa maana Mungu ni wa Milele Naye anaendelea kukua.

Kwa hiyo, asanteni sana. Nami ninawatakeni mjue, hakuna mhudumu wala mtu ulimwenguni, nimjuaye, mwanadamu yeyote, haidhuru ingekuwa ni nani, ila, ambaye nampenda kwa moyo wangu: ninawataka kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Ninashughulika kwa ajili ya mahali pamoja, huko juu, si kwa ajili ya dhehebu lolote.

Nilikuwa Mbaptisti wa Kimishenari, aliyewekwa wakfu kwenye Baptisti ya Kimishenari, na Daktari Roy E. Davis, kutoka Fort Worth, Texas. Nami nilikuwa . . . nilikaa kanisani. Kundi la ndugu wa—wazuri; nami ningali nitasema, "Wapo baadhi ya watu walio wazuri sana ulimwenguni, katika Kanisa la Kimishenari la Baptisti."

Lakini wakati nilipohudumiwa karama hii, wasingeweza kuipokea. Mchungaji hata alisema nimerukwa na akili. Mimi, nikiwa na elimu ya msingi, ningewahubiria wafalme, watawala wakuu, wafalme wakuu; na uponyaji na kadhalika. Yeye alisema, "Haiwezekani." Lakini ilitendeka, mnaona, maana Yeye alilifanya. Alisema, "Billy, utakuwa mtakatifu anayejifingirisha." Sijui kile nilicho mimi, bali ninamjua Yeye ninayeamini. A-ha. Ninaninii . . .

Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, alisema . . . mtu mzuri sana, akisafiri na mimi na Ndugu Jack Moore, William Booth-Clibborn; nafikiri ni mmoja wa wahubiri werevu sana niliopata kusikia, anaweza kuihubiri Injili katika, kikamilifu, katika lahaja saba.

Nami nikamwambia jambo fulani (kuhusu jambo fulani alilokuwa ametaja, juu ya jambo nililokuwa nimesema), nikasema, "Vema, hivyo ndivyo yasemavyo Maandiko hasa, Ndugu Booth."

Akageuka (kama mtu yeyote alipata kumjua, yeye ni mwanadiplomasia halisi, Mwingereza) naye akasema, "Kamwe huijui Biblia yako."

Nikasema, "Bali ninamjua Mwandishi Wake vizuri sana." Na hiyo ni . . . Mnaona?

Kwa hiyo, kumjua Yeye, ni Uzima. Na kwa hiyo—na kwa hiyo yeye . . . Hiyo ni kweli, mjue Yeye, kumjua Yeye, ni Uzima. Nami ninajua jambo fulani lilinipata. Siko vile nilivyokuwa. Kama vile maskini yule mama mweusi (kama hili litasamehewa, tafadhali, maana hapa si mahali pa mzaha, wala si mzaha, kwa kweli lilitukia), maskini mama mweusi, anasema, "Mimi taka kutoa ushuhuda."

"Simama, dada, ukatoe ushuhuda," nikasema.

Akasema, "Mwajua," kasema, "Mimi siiko jinsi ninavyotaka kuwa," kisha akasema, "Siiko jinsi ninavyopaswa kuwa," lakini, kasema, "basi siiko jinsi nilivyokuwa."

Alianza safari kwa vyovyote vile. Kwa hiyo hivyo ndivyo ninavyojisikia, pia. Mimi, si vile ninavyotaka kuwa, wala si vile ninavyopaswa kuwa, bali ninajua siko . . . siko nilivyokuwa. Jambo fulani lilitendeka kwangu yapata miaka thelathini na mitano iliyopita. Naye amekuwa moyoni mwangu tangu wakati huo. Nami nampenda kwa yote yaliyo ndani yangu.

Nami nawapenda. Ninawezaje kumpenda pasipo kuwapenda ninyi? Ninaye mvulana hapa mkutanoni, na mjukuu mdogo. Afadhali, kama mna pongezi zozote, muwape hao, badala yangu, maana mimi ni mzazi. Kwa hiyo, Mungu hujisikia vivyo hivyo. Kama hatuwezi kupendana sisi ambao tumeonana, tutampendaje Mungu, basi? Mnaona? Lazima kupendana, na kuheshimiana mmoja kwa mwingine.

Kama nikija hapa kuwadanganya ili kuwaingiza katika kitu ambacho ni mtego, ama chochote kile, kitu fulani, Mungu kamwe hawezi kukiheshimu. Angalieni kile angenifanyia mimi. Ninawafanyia nini watoto Wake? Kamwe nisingekuwa sawa na Mungu juu ya hilo. La.

Bali ninakuja kwa kuwa ninawapenda, Naye Mungu anajua hiyo ni kweli. Nami na—nataka kufanya kila niwezacho, ili kwamba furaha iliyowekwa huko juu kwa ajili yenu . . . Nafikiri ile meza kuu imeandaliwa, kila mmoja ana haki ya kuiendea.

Watu wengine husema uponyaji wa kiungu haupo. Ninajua upo. Mnaona. Mimi . . . Umechelewa sana kuniambia hilo. Unaona. Ninajua—ninajua ni kweli. Naye Roho Mtakatifu, na mambo hayo, ninajua ni ya kweli. Basi ni kwa nini ungesimama upande mmoja na—na ma—maskini kiazi baridi, umekishika mkononi mwako, ukikitafuna, huku chakula kingi mno kimewekwa kwa kila mmoja wa watakatifu wa Mungu. Unaona. Chote ni chetu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Shukrani milioni moja kwenu.

Na sasa, katika . . . Ninatumaini kurudi siku moja, Yesu akikawia. Sasa nadhani mnashangaa ni kwa nini . . . Mtu fulani alisema hivi majuzi . . . Nilisimama karibu na mtu maarufu sana. Ninampenda mtu huyo. Hakuna haja kwangu kumwita, kutolitaja jina lake. Yeye ni nanii wangu, mmoja wa marafiki wasiri wangu, Oral Roberts. Oral alikuja kwenye mkutano wangu. Ndugu Jack Moore alikuwa hapo. Alikuwa na maskini hema dogo chakavu limewekwa uwanjani, kule u—upande wa mashariki wa Jiji la Kansas, nami nilikuwa kwenye jumba la mikutano, kidogo kubwa kuliko hili. Akaja, akaketi pembeni, kasema, "Ndugu Branham, unafikiri Mungu angeyasikia maombi yangu?"

Nikasema, "Atayasikia maombi ya mtu yeyote."

2 Sasa mtu huyo hajui thamani yake mwenyewe, anajenga jengo la seminari la dola milioni hamsini, pamoja na ofisi ya dola milioni tatu. Nafikiri hiyo ni heshima, na mchango wa imani ya maskini mvulana mmoja, wa Oklahoma, kwa Mungu.

3 Tommy Osborn, alikuwa huko juu usiku huo wakati huyo mwendawazimu alipokimbilia jukwaani huko Portland, Oregon, kuniua. Naye akasema, "Mdanganyifu wee!" Kasema, "Ewe . . . " Akaniita tu kila kitu. Mtu mkubwa, mnene. Yapata wahubiri hamsini, jukwaani, wakamkimbia. Alikuwa ni mwendawazimu kutoka kwenye hospitali ya wendawazimu. Mikono mikubwa, minene. Urefu wa futi sita, karibu saba. Mikono mikubwa, minene. Nilikuwa na uzito wa ratili mia moja na ishirini na nane. Akakimbilia jukwaani, kasema, "Usiku wa leo, nitakurusha mpaka katikati ya mahali pale."

4 Nisingethubutu kumwambia lolote. Na kila mtu akarudi nyuma. Nami nikasimama tu wima. Usi—usijaribu kuingiza

mawazo yako; kama ukiyaingiza, utapotea. Nilisimama tu kimya. Ndipo nikajisikia mwenyewe nikisema hivi, hiyo ni, Roho Mtakatifu akilisema kupitia midomo yangu.

5 Kumbukeni, Mungu hutenda tu kazi kupitia kwa mwanadamu. Alimchagua mwanadamu. A—angalifanya Injili ihubiriwe kupitia kwa nyota, ama kupitia mitini, ama kupitia upepo, bali alimchagua mwanadamu. Hivyo ndivyo alivyopata kufanya, kumchagua mwanadamu. "Kuzifunua siri Zake," na kujua Kwake kimbele na kadhalika, "kwa watumishi Wake manabii," Yeye alisema.

6 Sasa, jamaa huyo alikuwa amesimama futi chache tu kutoka kwangu, naye alikuwa ametishia atakalofanya. Alionekana kama Goliathi. Na hapo Roho Mtakatifu akasema, "Kwa kuwa umelipa Neno la Mungu changamoto, usiku wa leo utaanguka miguuni pangu."

7 Vema, sasa mnaweza kuwazia, mtu mwenye hasira kama hiyo angewazia juu ya mtu mwenye uzito wa ratili mia moja na ishirini na nane, ukilinganisha na karibu ratili mia tatu za—za kama mlima uliosimama mbele yako, yale aliyowazia. Akasema, "Nitakuonyesha nitaangukia miguu ya nani," ndipo akagutua ngumi yake kubwa. Kamwe sikusogea; nilisimama tu pale. Naye akanijia, akajivuta nyuma namna *hii*, anipige.

8 Ndipo nikajisikia, si usemi wangu hata kidogo, kasema, "Shetani, mtoke mtu huyu." Sio kwa sauti kubwa kuliko hiyo.

9 Basi alipogutua ngumi yake nyuma; mikono yake ikaenda juu, macho yake yakatokeza, na kuzunguka-zunguka. Ulimi wake ukatokeza, na udenda ukaanguka kutoka kinywani mwake. Akazunguka na kuzunguka na kuzunguka, akaanguka chini na kuubana mguu wangu sakafuni.

10 Halafu huyu hapa polisi anajitokeza, nao walikuwa wakimsaka. Nilikuwa nimewaongoza polisi hao wawili kwa Kristo, huko nyuma kwenye chumba cha kuvalia nguo katika jumba hili kubwa la mikutano.

11 Na kwa hiyo nafikiri tulikuwa na yapata watu mia sita ndani, na karibu maradufu idadi hiyo huko nje. Kulikuwa kukinyesha mvua. Hao wakisimama, huku na huku mitaani, wakiwa na miavuli.

Basi akanibana sakafuni. Naye akasema, "Kwani amekufa?"

Nikasema, "La, bwana."

"Vema," kasema, "ameponywa?"

12 Nikasema, "La, bwana. Yeye humwabudu pepo huyo, unaona. Wala hakuna njia ya kumsaidia, hata kidogo, mpaka atakapoliondosha hilo kichwani mwake." Nikasema, "Lakini laiti mngemfingirisha aondoke miguuni mwangu, nipate kusogea." Mnaona?

13 Tommy Osborn akaona jambo hilo, ndipo akaenda nyumbani na kujifungia kabisa chumbani kwa siku tatu.

14 Akaendesha motokaa mpaka Jeffersonville. Ndipo akashuka akaja, maskini jamaa mdogo mwenye wasiwasi akikimbia karibu na gari lake. Akasema, "Unafikiri nina karama ya uponyaji?"

15 Nikasema, "Tommy, unaonekana kama mvulana mwenye mafanikio, na mtu ambaye angekuwa ni baraka kwa Ufalme wa Mungu." Nikasema, "Tommy, usifanye hivyo. Usiende ukiyawazia mambo hayo." Nikasema, "Unajua Mungu alikuita ukaihubiri Injili. Kama akikuita kuibubiri Injili, uponyaji wa Kiungu huambatana nao." Naye akaenda kule juu pamoja na Ndugu Bosworth.

16 Basi hivi majuzi nilisimama na kuangalia jengo lake, na, loo, jamani, dola milioni moja na nusu, ama chochote kile, mle. Nikaangalia kule, Oral alikuwa amesimama pale. Nilikuwa nikingojea. Nilikuwa niko kule. Oral alikuwa ni mzuri sana, na hao wote, wakinitembeza kule. Ndugu wazuri kweli!

17 Basi nikasimama pale, nikawaza. "Hebu fikiria, nilikuwa hudumani kabla hao hawajaanza. Hao, kila mmoja, anakwambia kwamba walipata uvuvio kutoka hapo." Ndipo nikawazia, "Ningechukia wao kuja ofisini mwangu." A-ha! Nina mashine ndopo ya kupiga chapa imewekwa pembeni mwa trela. A-ha. Mnaona? "Singetaka waione." Nikawaza, "Bwana, angalia hapa, angalia jengo hili kubwa lenye thamani ya dola milioni tatu, wanavyosema." Nami nikawaza.

18 Nikaangalia barabarani, nami nikaenda; ilisema, "makazi ya baadaye" ya *Nanii*. "Makazi ya baadaye."

19 Nami nikawaza. Lakini si—sisemi haya kwa kuwadharau ndugu hawa, bali yale tu niliyoambiwa. Nikawaza, kwani makazi yangu ya baadaye yako wapi? Kitu fulani kikasema, "Angalia juu." Kwa hiyo hilo ni zuri vya kutosha kwangu. Mradi tu. . .Nitayaangalia yangu Huko juu. Kwa hiyo sisemi hao hawatakuwako Kule, pia, mnaona, bali hiyo ilikuwa tu ya kunitia moyo, mnaona.

20 Nisingekuwa na akili ya kutosha kujua jinsi ya kushughulikia pesa kama hizo. Mungu anajua hilo, pia. Halafu basi vipi kama nilikuwa na wajibu mkubwa mno kama huo, je! mnafikiri ningeweza kuja hapa mahali hapa? Mnafikiri ningefanya mkutano wa siku tatu hapa kama Ndugu Roberts? Wakati, Ndugu Roberts anapaswa kuwa na kama elfu kumi kila siku. Mbona, ningeingia wazimu siku ya kwanza, kugharimia huo. Mnaona? Mbona, ninaweza kufanya mkutano ambapo kuna watu watano, ama watu wawili, ama mtu mmoja, ama niende popote anaponituma. Sina haja ya kitu chochote ila Yeye zaidi. Kwa hiyo hicho ndicho ninachowataka mkiombee, kwamba nitakuwa na zaidi Yake, kumjua Yeye. Bwana awabariki!

21 Kila umati, sasa, wana matabaka matatu ya watu: waaminio, wanaojifanya waaminio, wasioamini. Unao katika kila umati.

22 Yesu alikuwa nao katika Wake, nami niliwaonyesha hivi majuzi usiku jinsi ambavyo aliwabagua kwa kusema mambo pasipo kuyaelezea. Mnaona? Yeye hakusema ni *kwa nini* ingewabidi kula mwili Wake, *kwa nini* alikuja; *jinsi* angeshuka, Yule hasa aliyepaa juu. Wakati, hawa watu walijua Yeye alikuwa ni mwanadamu tu, kwanza kabisa alikuwa na jina baya, bali alisema hivyo kuijaribu tu imani yao.

23 Hao wanafunzi kamwe hawakusogea. Wasingeweza kulielezea. Lakini angalia kile Petro alichosema, "Bwana, twende wapi?" Mnaona, walikuwa wameliona Neno la Mungu kwa ajili ya siku hiyo, lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo, likithibitishwa. Wakasema, "Tunajua Hicho ndicho chanzo chake."

24 Mwangalieni yule mwanamke Mshunami, njia ile ile, wakati alipompata yule mvulana mdogo kutokana na baraka za Eliya. Yeye alisema, "Nitandikie nyumbu, wala usisimame hata nitakapokwambia." Mnaona? Naye akamwendea mtu wa Mungu. Wala hakujua. Bali alijua kama Mungu angeweza kumfanya nabii huyo kumwambia angempata mwana, angeweza kujua ni kwa nini Mungu akamchukua mwanawe. Naye aling'ang'ania katika kufanya hivyo. Nanyi mnakumbuka, yeye alidumu na imani ya—ya—yake mpaka akajua ni nini . . . ni nini kilicholisababisha. Ndipo Eliya akaenda, bila hata kujua la kufanya, akaenda huku na huku sakafuni; akauweka mwili wake juu ya mtoto huyo, naye akafufuka.

25 Mnaona, ni kwa kuwa watu wanaamini. Ha—hawawezi kueleza. Hakuna mtu anayeweza kumwelezea Mungu. Bali unapomwona Mungu akifanya jambo fulani katika Neno Lake, ambalo aliahidi kufanya!

26 Angalieni hao askari walevi wa Kirumi kwenye siku ile kabla tu kusulubishwa hakujatokea. Kumweka huko nje, na kumpiga kofi usoni na mashavuni, na mambo kama, kasema, "Sasa, ikiwa Wewe ni nabii, twambie ni nani aliyekupiga." Yeye alijua ni nani aliyempiga, bali haikumbidi kufanya vitimbi. Mnaona? Yeye tu—Yeye alininii tu . . .

27 Akasema, "Amin, amin . . . " Yohana Mtakatifu 5:19, sasa sikilizeni. "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe; ila lile ambalo amwona Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana." Kwa hiyo, kamwe hakufanya mwujiza mmoja mpaka Mungu alipomwonyesha, kwa ono, la kufanya, kulingana na Maneno Yake Mwenyewe. "Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe," si yale anayosikia, "bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana."

28 Hakuna nabii, hakuna mwonaji katika Biblia, aliyepata kufanya jambo moja kwa kubahatisha. Mungu huonyesha

kwanza. Kwa hiyo hakuna—hakuna mwili wa mwanadamu, si hata mwili wa Yesu Mwenyewe, unaoweza kujitukuza. Yote ni katika Mungu. Mungu ndiye huonyesha, kuonyesha, sisi tunafanya tu jinsi anavyotuonyesha na kutwambia. Kila mmoja wetu hufanya hivyo.

29 Kwa hiyo Bwana na awabariki sasa. Nami nitawauliza tena, alasiri ya leo, tunapolisoma Neno. . .Nanyi ni watu wazuri sana, ningeweza tu kusimama na kuzungumza nanyi na kuzungumza nanyi.

30 Bali ninataka kusema, tena, ninauaibisha Ujumbe ambao Mungu amenipa, kwa kukimbia tu humu. . .Tungekuwa na ibada tano, bali nafikiri tusingeweza kupata jumba hilo la mikutano, kwa hiyo ilitubidi tu kufanya nne; hapa siku tatu usiku, halafu ibada ya uponyaji. Ambapo, mnaona, hata hujui kukaribia kwa kwanza. Kwa hiyo labda siku moja, Mungu akipenda, mimi. . .na msaada wa Mungu na ushirikiano wenu enyi watu wema, ningetaka kurudi na kuwakusanya ndugu zangu wote, wote pamoja. Sisi, huenda likasikika kidogo ni la kuchekesha, bali, "Njoni, tukahojiane," asema Bwana. Hebu—hebu tuone hilo mpaka—mpaka wakati huo. Kama sitaweza kufanya hivyo, kumbukeni, nitakapowaona tena kwenye ng'ambo ya Mto, Mungu atashuhudia tena kwamba hii ni Kweli ninayowaambia. Ni Neno Lake.

31 Hivi si ningekuwa mnafiki, ninii—ninii. . .Ingenifaa nini? Ninaye mke na watoto nyumbani, wakilia kwenye simu, muda mfupi uliopita, "Kwa nini usije nyumbani?" Mnaona? Lakini kuna watoto wengine walio wagonjwa na wahitaji. Kuna wake wa wanaume wengine, na waume, wanaohitaji wokovu. Siwezi kufanya hivyo, kama ninatarajia kuvuka ule Mto. Mnaona, Huko nitaketi chini na kupumzika kidogo basi. Mpaka wakati huo, ninazeeka, na siwezi—siwezi kujisikia kama nilivyojisikia wakati nilipoanza miaka mingi iliyopita, bali na—naenda tu, kwa vyovyote vile. Kuenda tu, kwa vyovyote vile, kwa kuwa hii ndiyo nafasi ya mwisho nitakayoweza kufanya hivyo, katika maisha haya. Maisha yale mengine, hayatahitaji jambo hili.

32 Na tusimame sasa kwa heshima ya Neno Lake, tunapofungua Marko mlango wa 16. Nami nitaanza kusoma kwenye kifungu cha 9. Sikilizeni kwa makini, mkipenda.

33 Huu ndio ujumbe wa kumalizia. Huu leo ndio ujumbe wa kumalizia sehemu hii ya uamsho hapa. Na haya ninayosoma ndiyo Maneno ya kumalizia, mambo ya mwisho ambayo Yesu aliliambia Kanisa Lake kabla hajaondoka, Maneno ya mwisho mara baada ya ule ufufuo.

34 Mlango wa 16 wa Marko Mtakatifu, nitaanzia kwenye kifungu cha 9.

*Naye Yesu alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwamba alimtoa pepo saba.*

*Huyo akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa pamoja naye, nao wakali wanaomboleza na kulia.*

*Walakini hao . . . waliposikia yu hai, . . .*

35 Wazia tu hilo, "hao waliposikia kama yu hai." Loo, jamani! Natumaini tunaweza kusikia jambo lilo hilo leo hii, na kujua kwamba Yu hai. A-ha.

*. . . waliposikia kama yu hai, naye amemwona, hawakusadiki.*

*Baada ya hayo akawatokea* (wengine) *miongoni mwao, ana sura nyingine; nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.*

Hao walikuwa ni Kleopa na rafiki yake, wakienda Emau.

*Nao wakaenda zao wakawapa habari wale wengine; wala hao hawakuwasadiki.*

Baadaye, *baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.*

Nashangaa kama angefanya jambo lile lile kwetu sasa? Mnaona?

*Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*

*Aaminiye na kubatizwa ataokoka; . . . asiyeamini, atahukumiwa.*

*Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu hao watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;*

*Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono* yao *juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*

*Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.*

*Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, . . . kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo! Amina.*

36 Sasa somo langu, alasiri ya leo, nitalitoa hapa: *Kesi Ya Mahakamani.*

Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu.

37 Baba yetu wa Mbinguni Mwenye rehema, tunakuomba sasa kulichukua Neno Lako; nasi tunapoleta, alasiri ya leo, kesi hii ya Neno Lako, tunaomba ya kwamba tutauhisi Uwepo wa Yesu aliyefufuka, na jalia tusiwe wavivu sana. Na kama ulivyowaambia wale uliposema nao wakienda zao Emau, jinsi ambavyo Wewe ulinena nao na ukawaambia ya kwamba walikuwa . . . "Kwa nini walihofu? Kwa nini walihuzunika?"

38 Nao wakasema, kwamba, "Hapana budi wewe ni mgeni." Kisha wakamwambia kwamba . . . "Yesu wa Nazareti, ambaye alikuwa mtu nabii."

39 Na hapo walipokuita Wewe nabii, basi ilipasa hata na zaidi kwamba inakubidi kwenda kwenye Neno, ukiwa ni nabii, kwa kuwa Neno humjia nabii. Ndipo ukawageukia, na kusema, "Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito kuamini, ya kutokuamini yote waliyosema manabii kumhusu Kristo, jinsi ambavyo inampasa kupata mateso haya yote uliyosema, kisha aingie katika Utukufu Wake." Ndipo akaanza kutoka Agano la Kale, huko nyuma kabisa mwanzoni, akawaelezea yale manabii walikuwa wamesema kumhusu Yeye Mwenyewe. Lakini, hata hivyo, wangali hawakufahamu.

40 Ila mara walipoingia ndani ya jengo, milango ikiwa imefungwa, basi Wewe ulifanya jambo fulani jinsi tu ulivyofanya kabla hujasulibishwa, ndipo macho yao yakafumbuliwa. Ukatoweka upesi machoni pao. Nao wakakimbia na kuwaambia hawa, walioketi chakulani, chakula cha jioni. Nawe ukawakemea kwa kutokuamini Kwao, wakati Wewe ulipotokea ukutani na kuwaambia ya kwamba iliwapasa kukuamini, na ugumu wa mioyo yao.

41 Na jinsi ambavyo wanafunzi hawa walifurahia kwa kuwa ulijitambulisha, kwa kuwa ulifanya jambo fulani sawasawa na ulivyofanya kabla ya kusulibishwa Kwako. Walijua huyo alikuwa ni Wewe; yeye yule jana, leo, na hata milele.

42 Ee Mungu, naomba, leo hii, ufanye hivyo tena. Njoo miongoni mwetu. Nawe uliahidi mambo haya kwa ajili ya siku za mwisho. Basi jalia mioyo yetu isishushwe sana na . . . na theolojia mamboleo na mambo ya ulimwengu, hata tutashindwa kukuona Wewe. Fungua ufahamu wetu, macho, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

43 Sasa, natumaini ya kwamba kuonekana kwa ufufuo Wake uliothibitishwa juma hili, yale machache ambayo tumeona, kwa kuwa ni mara yenu ya kwanza, huenda mkashuku kidogo, kwa kuwa jambo pekee ambalo mmeona ni sehemu ndogo tu. Bali halijakosea hata siku moja, katika makumi elfu mara maelfu. Halijakosea kamwe. Ni wangapi hapa ndani walio shahidi wa jambo hilo, inueni mikono yenu, ambao wameninii . . . Mnaona? Kamwe, haidhuru ni taifa gani, wapi, mahali, halijasema lolote

lingetukia ila lile lililotukia vivyo hivyo hasa. Kwa hiyo, hakuna kitu kinachoweza kuwa sahihi kiasi hicho isipokuwa Mungu, peke yake. Mnaona? Hakika.

44 Lakini, hakika, halina budi kuonekana la kidanganyifu. Halina budi kuwa hivyo. Ndivyo lilivyofanya katika siku Zake, na kadhalika. Hata kuzaliwa Kwake, na kila kitu kingine, kilionekana kidanganyifu. Mungu hufanya hilo apate tu kuijaribu imani ya watu Wake.

45 Sasa, alasiri ya leo, nilifikiri isingekuwa kweli zaidi . . . Na baada ya kuonekana Kwake mbele zetu na kutembea kote jengoni na kuyatambua mawazo ya moyo. Nami nimetumia tu Maandiko matatu ama manne madogo, pamoja nanyi.

46 Ambayo, Mungu anajua ya kwamba Maandiko yote yanaungana pamoja. Hakuna kosa moja katika yoyote Yake. Hakuna moja linalohitilafiana na lingine. Sasa, watu husema yanapingana. Nimetoa mshahara wa mwaka mmoja kwa yeyote atakayenionyesha mimi, ambapo Neno linajipinga Lenyewe. Halijipingi. Kama linajipinga, halina faida kwangu. Halina budi kuwa ni Kweli kabisa.

47 Sasa, Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kitu fulani. Kama akiuhukumu kwa kanisa, basi ni kanisa lipi? Maana, moja linahitilafiana na lingine. Bali atauhukumu kwa Yesu Kristo. Biblia ilisema hivyo. Naye Kristo ni Neno. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, na Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu." Yeye aliuhukumu katika siku za Nuhu, Naye aliuhukumu katika siku za Musa. Aliuhukumu katika kila siku, na siku Yake, na hata kwenye siku hii, kwa Neno lile lile lililoahidiwa la wakati huo. Ama tuliamini, au tusiliamini, bali Yeye anawajibika kulifanya Neno Lake kweli. Mnajua, katika Mathayo 12 pale, ilisema ya kwamba, ya kwamba . . .

48 "Ingawa alikuwa amefanya mambo mengi sana, hata hivyo watu wasingeweza kuamini. Kwa kuwa, Isaya anasema, 'Wana mioyo, hawawezi kufahamu; macho, hawawezi kuona; masikio, hawawezi kusikia.'" Ilibidi litimizwe.

49 Na vivyo hivyo hili halina budi kutimizwa. "Watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiowapenda walio wema; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake, Nguvu za Mungu yule waliye na mfano Wake." Ni jambo la kuhuzunisha jinsi gani! Vipi kama huyo alikuwa ni wewe? Wazia juu ya mwanamume ama mwanamke asiyeweza kuamini hilo. Vipi kama ilikuwa ni wewe? Liwazie tu. Ni—ni la kuhurumiwa, si la kudharauliwa, bali kuhurumiwa. Ni la Kweli kabisa. Angalieni sasa.

50 Leo hii nitaita kile tungeita . . . kwa dakika chache sasa, kabla hatujawaombea wagonjwa. Nasi tutajaribu tuwe

tumetoka hapa katika dakika arobaini zijazo, ikiwezekana, bali ninataka tu kuwa na kesi ndogo kwanza.

51 Na sasa kesi ni ya kwamba, leo hii, katika kesi hii ya mahakamani. Sasa kama mtasikiliza tu kwa makini, na kuzingatia akilini yale ninayojaribu kusema. Haitachukua muda mrefu. Kesi hii, ni, "Neno la ahadi za Mungu dhidi ya ulimwengu." Sasa ke—kesi haiwezi kuitwa isipokuwa iwe ni kwa sababu fulani. Inakubidi kuleta kesi. Nayo kesi iliyoletwa kwenye chumba hiki cha mahakama alasiri ya leo. . . Sasa ninawatakeni, kila mmoja, na—nawaapisha, mwisikilize kesi hii. Sasa kesi hii, ni, "Neno la ahadi za Mungu dhidi ya ulimwengu," kesi hii.

52 Na sababu ya shtaka hili, ni, "Uvunjaji wa ahadi." Je! mnaweza kunisikia vema? Inueni mikono yenu, kama mko huku kila mahali sasa, mnaweza kusikia. Sh—shtaka, ni, "Uvunjaji wa ahadi. Mungu alitoa ahadi wala hakuishughulikia." Neno la Mungu lilitoa ahadi, kwa hiyo Yeye ananinii—anapelekwa kwenye kesi mahakamani. "Uvunjaji wa ahadi."

53 Sasa, mwendesha mashtaka daima huiwakilisha serikali, kama ninaelewa mahakama vizuri. Kwa hiyo mwendesha mashtaka katika kesi hii anauwakilisha ulimwengu, naye mwendesha mashtaka ni Shetani. Yeye anauwakilisha ulimwengu kwa sababu ulimwengu ni wake. Naye anauwakilisha ulimwengu, naye ndiye mwendesha mashtaka wao.

54 Mshtakiwa katika kesi hii ni Mwenyezi Mungu, mshtakiwa.

55 Na sasa mshtakiwa sikuzote huwa na shahidi wa utetezi. Naye shahidi wa utetezi katika kesi hii ni Roho Mtakatifu. Na sasa tunaenda kuninii . . .

56 Naye mwe—mwendesha mashtaka pia ana mashahidi fulani katika kesi hii, nami nitawataja. Basi mmoja wao ni Bw. Asiyeamini, huyo mwingine ni Bw. Mwenye Kushuku, na mwingine ni Bw. Mkosa Subira. Hawa ndio wanaojaribu kuleta hukumu juu ya Mungu.

57 Sasa tuna ninii . . . wa—wahusika wote sasa wameitwa. Nasi tuko mahakamani, kwa hiyo tutaituliza mahakama. Vema. Utaratibu—utaratibu ni, Mahakama imeagizwa kubadilisha, ama kutulia.

58 Basi mwendesha mashtaka sasa atamwita shahidi wake wa kwanza kutoa ushahidi. Naye shahidi wake wa kwanza kusimama ni Bw. Asiyeamini.

59 Nalo shtaka lake ni, kwamba, "Neno la ahadi la Mungu si la kweli kabisa." Hilo ndilo lalamiko lake, huyo shahidi wa kwanza. Anadai kwamba yeye ni mwaminio; ingawa siye; bali anadai kuwa ni mwaminio. Basi anadai kwamba alikuwa "akihudhuria hapa, wakati fulani uliopita, mkutano,

unaodhaniwa, ni wa Roho Mtakatifu, ambapo watu walikuwa wakiwawekea watu mikono, na kutoa haki zao za Kimaandiko kufanya jambo hili, wakisoma kutoka katika Marko 16," ambapo nimesoma sasa hivi. "'Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.'"

60 Bw. Asiyeamini anashuhudia, naye anasema, kwamba, "Nilikuwa nimewekewa mikono na huyu, wanayemwita, mhubiri aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akaweka mikono yake juu yangu, kulingana na Marko 16, ile ahadi aliyofanya Mungu. Naye mtu huyo akasema alikuwa ni mwaminio. Na wengi walidai kuponywa. Naye akaweka mikono yake juu yangu, na hiyo imekuwa ni miezi miwili iliyopita, wala hakuna kitu kilichotendeka. Kwa hiyo, ahadi hiyo si ya kweli." Vema. Tunamwomba Bw. Asiyeamini ashuke chini.

Mwendesha mashtaka, Shetani, anamwita shahidi wake anayefuata.

61 Shahidi anayefuata anasimama, ni Bw. Mwenye Kushuku. Sasa anashuhudia. Alisema, "Nilienda kanisani. Nilikuwa mgonjwa, nami nilienda kwenye kanisa ambalo linadhaniwa lina mchungaji mtauwa mle, ambaye alikuwa anaamini Neno la Mungu. Naye alikuwa na chupa ndo—ndogo ya mafuta dawatini mwa—mwake. Nao watu wake wote waliokuja kule, waliotaka kuombewa, aliwapaka mafuta, akisoma ahadi hiyo kutoka kwa Neno la Mungu, katika Yakobo 5:14.

62 "Akalisoma Neno, na kusema, 'Akiweko mgonjwa yeyote miongoni mwenu, na awaite wazee wa kanisa, na wamtie mafuta na kuwaombea, kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo, Naye Mungu atamwinua. Kama wamefanya dhambi yoyote, watasamehewa.' Na sasa," akasema, "nilimwacha mchungaji huyu, ambaye nilikuwa nimesikia shuhuda zake kutoka kwa wengine, anitie mafuta, huku akinisomea Maandiko, kutoka kwenye ahadi ya Mungu. Na hiyo imekuwa ni zaidi ya mwezi mmoja uliopita, nami ningali mgonjwa tu kadiri nilivyokuwa wakati aliponitia mafuta." Kwa hiyo, hilo ndilo lalamiko lake. Hebu Bw. Mwenye Kushuku ashuke chini.

63 Basi mwendesha mashtaka, Shetani, anamwita shahidi wa—wake anayefuata. Shahidi wake anayefuata ni Bw. Mkosa Subira. Huyo ni haini. Mnaona? Samahani kwa tamshi hilo. Mnaona? Anakufanya tu, anakufanya uwe na wasiwasi sana, hujui unalofanya. Mnaona?

64 Bw. Mkosa Subira, yeye anadai kwamba yeye. . . "Siku moja, wakati akisoma Biblia. . . " Hawa wote wanadai kwamba ni waaminio sasa. Nao. . . Anadai kwamba alikuwa "akisoma Biblia," naye "akapata kifungu cha Marko 11:22 na 23, ambapo Yesu Mwenyewe alifanya ahadi, kwamba, 'Ukiuambia mlima huu "ng'oka," wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale umesema yatatimia, yatakuwa yako.' Na

tena anasema, 'Kama ninyi, mnapoomba, aminini mnapokea mnachoomba.'" Sasa anasema, "Nimekuwa m—mlemavu miguuni mwangu, kiwete miguuni mwangu, kwa miaka thelathini. Nami niliikubali ahadi hiyo, miaka mitano iliyopita, wala hakuna kitu kilichotukia tangu wakati huo. Ningali kiwete tu kama nilivyopata kuwa." Sasa, sasa mwende-. . . Ndipo anashuka chini.

65 Sasa kwa namna fulani mwendesha mashtaka hana budi kuiendesha kesi. Kwa hiyo mwendesha mashtaka, ambaye ni Shetani, anauambia umma, mnaona, "Watu hawa wanadai ni waaminio. Basi Mungu hana haki ya kuweka ahadi za kijinga kama hizo katika Neno Lake, wakati Yeye hazitimizi." Mnaona, yeye anamshtaki Mungu. "Yeye aliweka ahadi hizi katika Neno Lake, kwa ajili ya watoto Wake waaminio. Nao watoto Wake waaminio walipanda hapa wakashuhudia ya kwamba wamekubali dai hili, ambalo amefanya katika Neno Lake, kwamba ni Kweli, wala hawana matokeo Yake hata kidogo."

66 Kwa hiyo anamshtaki Mungu, akijaribu kupata kesi dhidi Yake, kusema kwamba, "Mungu ameweka kitu fulani katika Neno Lake, kwa ajili ya watoto Wake waaminio, wala Yeye hatimizi aliyoahidi." Pia anadai ya kwamba, kwamba, "Yeye sio mwenye haki kwa kutoa ahadi kama hiyo kwa watu, kwa watoto wake waaminio, huku hawezi kutimiza yale aliyosema angetimiza." Sasa mwendesha mashtaka anaonyesha kesi ngumu hapa dhidi ya mshtakiwa. "Hana uwezo wa kulitimiza, kwa kuwa tunao mashahidi hapa, kwamba, 'Yeye halitimizi Neno aliloahidi.'"

67 Naam, mwendesha mashtaka anaendelea kuzungumza. Mwendesha mashtaka anasema, ambaye ni Shetani, "Hata hivyo, Mungu ameahidi, kwamba, 'Mambo yote yanawezekana kwa waaminio.' Mungu amesema hivyo katika Neno Lake." Mwendesha mashtaka ana—ana—anafunga kesi yake sasa, mnaona. Anafikiri ameshinda kwa kuwa hao mashahidi watatu waliotoa ushahidi, na kuyaendea Maandiko, na wakayanukuu Maandiko vizuri, na kila kitu jinsi wa—wamefanya. Na sasa mwendesha mashtaka anafunga hizo sehemu ndogondogo, ambazo, "Mungu ameahidi kwamba, 'Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.'"

68 Hata hivyo, mwendesha mashtaka anazungumza tena, Shetani, na kusema, "Mungu anaahidi kuwa hai akiisha kusulibishwa. Anaahidi, Yeye anaahidi angali yu hai. Na, pia, Yeye anaahidi katika Maandiko Yake, Waebrania 13:8, kwamba, 'Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.' Naye hawezi kuunga mkono ama kuzitimiza ahadi Zake." Anaishindilia, kwelikweli, kusudi kusiwe na na—nafasi ya kuiepa. "Hawezi kulitimiza. Mungu hawezi kulitimiza Neno Lake," kwa maneno mengine. "Anadai ya kwamba amefufuka katika wafu.

69 "Anadai, pia, katika Yohana 14:12, ya kwamba, 'Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.' Hajaweza kulitimiza hilo. Alisema pia, katika Maandiko, 'Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo mtaniona. Kwa kuwa Mimi ni hai, mnaishi pia.'

70 "Angalieni tena, Yeye anadai kuwa katika Marko... mlango wa—wa 17, akinena kuhusu siku za Sodoma, ambazo tunaishi sasa, 'kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,' kwamba mandhari ya ulimwengu yangekuwa katika hali ile ile. Na kwamba Mungu angeshuka chini, akiwa ni Neno lililodhihirishwa katika mwili hapa duniani, na angeweza kufanya mambo yale yale ambayo—ambayo—ambayo Mungu alifanya, ambaye alikuwa ni mtu katika umbo la mwanadamu, ambaye aliitwa, na Ibrahimu, 'Elohimu.' Naye Yesu alisema, 'Wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa' katika siku za mwisho, kwamba Yeye angejifunua Mwenyewe kwa njia ile ile iliyochukuliwa katika siku za Lutu, akionyesha mandhari hiyo.

71 "Yeye pia anaahidi, kwamba, 'Atakuwa pamoja nasi, hata ndani yetu, hata ukomo, ama mwisho wa ulimwengu.' Na pia anadai, kwamba, 'Mbingu na nchi zote zitashindwa, bali Neno Lake halitashindwa kamwe.'"

72 Sasa nafikiri mwendesha mashtaka anafikiri ameikaza kesi yake vizuri sana. Anao mashahidi wa kuthibitisha ya kwamba Neno hili si la Kweli.

73 Sasa ninyi ni hakimu na baraza la wazee wa mahakama pia, alasiri ya leo. Ninyi, mioyo yenu, ndio baraza la wazee. Na matendo yenu ndiyo hakimu. Ninyi, ninyi ni vyovyote uamuzi wenu wa baraza la wazee ulivyo. Mtatenda kama uamuzi wenu ulivyo. Mnaona? Itawabidi kufanya hivyo, maana matendo yenu yananena kwa sauti kuu kuliko maneno yenu. Mnaona? Hiyo ni kweli. Unaweza kusema jambo fulani, bali ikiwa hulimaanishi, huwezi kulitenda. Mnaona? Matendo yenu yatatoa sauti kuu kuliko maneno yenu. Angalieni.

74 Sasa hebu mwendesha mashtaka ashuke chini. Ametoa, alikuwa na mashahidi wake, nao wameshuhudia. Naye mwendesha mashtaka ameliweka Neno hapa nje na kulifunga jinsi tu anavyolitaka. Kwa kuwa, yeye anafikiri ameifunga kesi hii kabisa sasa, kwa hiyo hebu mwendesha mashtaka pamoja na mashahidi wake washuke chini kutoka kizimbani.

75 Sasa tutaita shahidi wa utetezi, Roho Mtakatifu. Mwajua, kama kuna mshtakiwa, hapana budi pawe na shahidi wa utetezi. Kwa hiyo tutamwita shahidi wa utetezi amtetee mshtakiwa, Roho Mtakatifu.

76 Jambo la kwanza Roho Mtakatifu analosema wakati akipanda juu, ni hili. Anataka kumhamasisha mwende-... mwendesha mashtaka, yule anayeendesha kesi iliyoshtakiwa, kwamba, "Mwendesha mashtaka amelifasiri Neno vibaya kwa

watu, sawasawa tu na alivyomfanyia mwanadamu wa kwanza, Hawa, katika bustani ya Edeni. Yeye amewafasiria watu Neno vibaya." Naye Roho Mtakatifu, shahidi wa utetezi, anawatazamisha jambo hili.

77 "Angalieni, alisema hilo, mwe—mwendesha mashtaka amesema, ya kwamba, 'Ahadi hizi ni kwa ajili ya waaminio.' Na, kwamba, waaminio ndio tu walioahidiwa ahadi, sio wasioamini na wenye kushuku." Shahidi wa utetezi, madai Yake, ni kwamba, "Mungu alisema waziwazi kwamba ilikuwa ni kwa ajili ya waaminio; na anawatazamisha kwamba kila mmoja aliyetoa ushahidi, akilipinga Neno, alikubali ya kwamba wengine walidai kuponywa." Mnaona? Kwa hiyo hilo linamtupilia mbali sasa, mnaona, bali hebu tuendelee na kesi hii kitambo kidogo.

78 Naye shahidi wa utetezi anapaswa kujua kama hao ni waaminio au la, kwa kuwa Yeye Ndiye anayelihuisha Neno. Anajua kama wanaamini au hawaamini. Sivyo? [Kusnyiko linasema, "Amina."—Mh.] Anapaswa kujua. Anajua kama hao ni waaminio au la, kwa kuwa Yeye pekee ndiye anayeweza kulitia Neno Uzima. Hapa ungekuwapo mwili wangu bila roho, ningekuwa mfu; lakini uhai tu ndio unaoweza kuuhuisha mwili huu ukasogea. Na Roho Mtakatifu Ndiye tu anayeweza kulihuisha Neno. Yeye Ndiye tu anayeweza kulifanya litende kazi, Naye anapaswa kujua kama hao ni waaminio ama sio. Na kinyume na ushuhuda wao wenyewe ambao walisema, "Wengine walidai kuponywa, na wengine wakadai kuyaona mambo haya," bali wao hawakuyaona. Sasa, mnaona, shahidi wake tayari amehukumiwa.

79 Lakini, sasa, Yeye hulihuisha Neno. Na tena anataka kuita usikivu wenu kwa neno la mwendesha mashtaka, ama shtaka linalojadiliwa. "Yeye kamwe hakuweka wakati wowote kwa ajili ya uponyaji huu. Alisema, 'Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa huyo. Mungu atamwinua.' Alisema, 'Wataweka mikono juu ya wagonjwa.' Wala hakusema wangeruka juu papo hapo na kuponywa. Alisema, 'Watapata afya, kama wakiamini.' Mnaona, kunukuu Neno vibaya! Mnaona?"

80 Nafikiri tuna shahidi mzuri wa utetezi. Sasa, hapo, Yeye anapaswa kujua kama wanaamini ama hawaamini. Angeweza kusema hilo. Na hakika Yeye—Yeye huyasahihisha Maandiko hapa, kwa kuwa shahidi wa utetezi daima alifanya hivyo, kulingana na maneno ya Biblia. Neno daima hujisahihisha Lenyewe.

81 Nasi tunaona ya kwamba Yeye alisema, kwamba, "Shetani, amelinukuu Neno vibaya kwa huyo asiyeamini, wala huyo asiyeamini hakujua tofauti. Lakini Yeye aliyeliamini, alijua jinsi lilivyosema hasa, na kulishikilia." Mnaona? Mnaona? Hayo madai yao, wasingeweza kuyathibitisha. Bali waliyadai, wenyewe, nao walikuwa.

82 Kama vile tunavyodai kwamba tumeokoka. Hao wanasema, "Vema, nionyeshe jinsi ulivyookoka." Maisha yangu yanathibitisha nimeokoka. Jinsi ninavyotenda, inathibitisha kama nimeokoka ama sijaokoka. Haidhuru ninashuhudia jinsi gani kulihusu *hapa*, mtajua jinsi ninavyoishi kama nimeokoka ama sijaokoka.

83 Ni vivyo hivyo na uponyaji. Ukiukubali na kuuamini, utatenda jinsi hiyo. Kutakuwako na badiliko kubwa ndani yako! Hakuna kitu kinachoweza kuuondoa moyoni mwako, si zaidi ya wokovu wako. Ni Neno la Mungu. Huna budi kulikubali juu ya msingi ule ule.

84 "Kwa imani unaokolewa." Yesu alimwambia yule mwanamke aliyeligusa vazi lake, Yeye alisema, "Imani yako imekuokoa." Sasa, mimi si msomi kwa vyovyote vile, bali nimeyachunguza maneno machache. Sasa hilo neno hapo linatokana na neno la Kiyunani *sozo*, ambalo maana yake ni "kuokoka," kama tu kuokolewa kimwili ama kuokolewa kiroho. "Umeokolewa, sozo." Alimwokoa na kaburi la kabla ya wakati wake, sawa tu na anavyokuokoa na kuzimu. Sozo, neno lile lile la Kiyunani linatumika. Angalia, "Imani yako imekusozo, imekuokoa na magonjwa uliyokuwa nayo." Angalieni, neno lile lile kila wakati.

85 "Tena kuvuta usikivu sasa, mwendesha mashtaka amelinukuu Neno vibaya, wala Mungu hakusema wangeruka, upesi sana, mara walipowekewa mikono. Lakini Yeye alisema, 'Waaminio, watapata afya.' Hiyo ni kusema, kama anaamini! Ni kwa waaminio pekee.

86 "Na tena sha—shahidi wa utetezi anataka kuita usikivu, mahakama alasiri ya leo, kwamba, Mungu alisema kwamba Neno Lake lilikuwa ni mbegu. 'Neno ni mbegu ambayo mpanzi alipanda.' Ikiwa udongo huu, Mbegu ikianguka kwenye udongo mzuri, ulio na rutuba ya kutosha ndani yake kuifanya Mbegu hii ichipuke, kuihuisha, itaishi."

87 Sasa wakati mtu anapopanda mbegu. Kama wewe ni mkulima, ama unajua chochote kuhusu kupanda mbegu yoyote; kama ukipanda mbegu leo, mahindi kidogo, tuseme, uyaweke shambani mwako. Halafu kesho yake asubuhi uende na kuyachimbua na kuyaangalia, na kusema, "Vema, hamna tofauti kwake." Kisha uyapande tena. Na kesho yake, urudi, uyaangalie, na kusema, "Hamna tofauti kwake." Kamwe hayatachipuka. Hayawezi kuchipuka. Ulipoyachimbua, uliiharibu picha papo hapo. Inakupasa kuyakabidhi kwa ardhi, halafu ni jukumu la ardhi kufanya yaliyosalia.

88 Na kila wakati unapoangalia dalili zako, ushuhudie juu yake, uzilalamikie, Mungu kamwe hawezi kukuponya. Zikabidhi kwa Mungu na uliamini Neno Lake. Atayatimiza. Kama yanachipuka, kama ni chochote yanachofanya, hujali.

Mungu aliliahidi, na kimsingi umepata uponyaji wako wakati unapoukubali. Uko katika umbo la mbegu.

89 Kama nilikuomba mwaloni, nawe ukanipa mbegu yake, kimsingi nina mwaloni. Na kama nilikuomba suke la mhindi, nawe ukanipa punje ya mhindi, kimsingi nina suke la mhindi. Basi ninaiweka ardhini, na kuimwagilia maji, na kuiondolea magugu yote, ambayo yangezinyonya nguvu kutoka ardhi iliyoizunguka, ninayang'oa magugu. Basi itakua moja kwa moja, kwa kuwa imewekwa, na ni mbegu iliyorutubishwa. Sasa kama mbegu haijarutubishwa, haitachipuka. Lakini kama mbegu ina chembe ya uhai ndani yake, hakuna kitu kinachoweza kuifanya isikue.

90 Mtu fulani alisema, "Unawazia nini juu ya ufufuo?"

91 Toka hapa nje wakati wa baridi kali, mwaga saruji kidogo uani mwako, halafu nyasi zako zilizoshikana kabisa ziko wapi mwaka ujao wakati majira ya kuchipua yanapokuja? Kando ya njia. Mnaona, wakati mwanga huo wa jua, na ulimwengu unapozunguka na kufikia mahali pake upate kuangaziwa na hilo jua tena, hakuna njia tena ya kuuficha. Uhai hujifanyia njia. Unapenya chini ya saruji hiyo, na kadhalika, na kutokea moja kwa moja kando ya njia hiyo, na kukichomoza kichwa chake juu, katika kumsifu Mwenyezi Mungu. Jua, j-u-a, huudhibiti uhai wote wa mimea.

92 Naye M-w-a-n-a hudhibiti Uzima wote wa Milele. Kwa kuwa, Yeye, na Yeye pekee, yuna Uzima wa Milele. Huwezi kuuficha! Inabidi kuwe na ufufuo. Sijali uko wapi, unakuja, kwa vyovyote vile.

93 Nawe huna budi kuponywa kama unaliamini na kulikubali. Ni mbegu ambayo mpanzi alipanda, nayo ikaanguka ardhini. Na kama ikija . . . Zingine zilianguka kwenye miamba, mwajua, hazikuwa na mzizi; zingine zikaanguka kwenye miiba na masikitiko, nayo yakazisonga. Lakini zingine zilienda ambapo hapakuwapo na magugu na miiba na miamba.

94 Sasa inategemea kile ambacho wewe . . . Ukimwacha asiyeamini fulani kuingia nyumbani mwako, ama—ama mtu asiyeamini akwambie, "Mbona, kuna upuuzi ule, hamna—hamna kitu kama Hicho," unayaachilia magugu yaingie. Kataa hilo!

95 Useme, "Mungu alisema hivyo! Hilo latosha. Nimeponywa kwa kuwa ninaamini hilo moyoni mwangu." Na hiyo imani ikikaa pale, na kutokuamini kote kumeondolewa kwake, halina budi kulitoa. Hiyo ni kweli.

96 Sasa, shahidi wa utetezi anataka kuita mashahidi wa—wachache jukwaani. Tunaweza kuwa na wakati wa kufanya hivyo? Shahidi wa utetezi anataka kuita shahidi sasa, mashahidi Wake, kama vile mwendesha mashtaka alivyomwita shahidi wake. Shahidi wa utetezi atamwita, kwanza, nabii Nuhu, na

kumwacha atoe ushahidi. “Nuhu, unataka kusema nini sasa, alasiri ya leo, kulihusu?”

97 Akasema, “Niliishi katika wakati wa kisayansi uliopita sayansi ya wakati huu. Kamwe hakukuwa kumewahi kunyesha juu ya nchi. Mungu aliitia nchi maji kwa mimea, na kadhalika, kwa chemchemi zilizokuwa chini ya ardhi. Lakini siku moja Mungu alinijia, na akaniambia itanyesha maji kutoka angani. Nikautoa ujumbe wangu. Kisha akaniambia nijenge safina. Hilo nikafanya, na akasema itanyesha maji kutoka angani.

98 “Basi Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, na hao jamaa wote wanaoketi pale, walinidhihaki, na kunicheka, kwa kuamini mwujiza kama huo, wakati imethibitishwa kisayansi hamna maji huko juu. Wangeweza kurusha kwenye mwezi; wangeweza kurusha kwenye nyota. Wangeweza kufanya mambo ya namna hiyo, walijenga vitu wakati huo ambavyo hatuwezi kuvijenga leo hii, kwa hiyo wakathibitisha, kisayansi, hakukuwako na mvua yoyote kule juu.”

99 Lakini Nuhu akasema, “Mungu aliniambia itanyesha. Nami nikaamini, kama Mungu alisema hivyo, Yeye anaweza kuweka maji huko juu, kwa hiyo nikautangaza kwa nguvu. Bw.—Bw. Kutokuamini akanidhihaki, Bw. Mwenye Kushuku akanishuku. Bw. Kukosa Subira! Niliutangaza kwa nguvu, mpaka nikaijenga safina. Kila siku walikaribia, na kusema, ‘Vema, nadhani itanyesha leo? Ha-ha-ha!’”

100 Mnaona, vile vile, “Nilidhani ulikuwa mzima. Nilifikiri utapata afya.”

101 “‘Kwani mvua iko wapi? Mwajua, hata hivyo, nabii Nuhu, kwa kuwa unadhaniwa kuwa ni nabii, ulisema hivyo.’” Sasa kumbukeni, hao si wale...Hao ni watu wanaojifanya ni waaminio. La, Bw. Kutokuamini na Bw. Mwenye Kushuku, na hao ni, wanatoa dai kwamba ni waaminio. “‘Vema, nabii, Nuhu, daima tulijua wewe ni nabii wa uwongo, maana una mawazo ya kipumbavu yasiyoambatana na sayansi. Hayaambatani na mwelekeo wa kisasa. Unaona, wewe, wewe husikilizani na wachungaji wetu. Kuna kasoro. Tunajua kwamba kwa kweli wewe si nabii. Lakini ulisema itanyesha, hiyo ilikuwa ni mwezi mmoja uliopita, hamna mvua bado.’

102 “Miaka miwili ikapita, ‘Aise, aise, nabii, nilifikiri ulisema ya kwamba Mungu alisema hivyo?’

“Kweli alisema hivyo.

“‘Vema, miaka miwili imepita!’”

103 “Miaka mitano, miaka ishirini, miaka hamsini, safina imekamilika.” Nuhu alikuwa ameketi mlangoni. “Huyu hapa Bw. Mwenye Kudhihaki anakuja, Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, Bw. Mkosa Subira, ‘Vema, sasa, iko wapi mvua?’

104 "Mungu alisema itanyesha. Hakusema ni lini. Alisema, 'Itanyesha.' Hakusema ni lini. Alisema tu, 'Itanyesha. Jenga safina. Utaponea humo. Itanyesha.' Hakusema itanyesha lini. Alisema, 'Itanyesha,' ndipo nikaijenga safina.

105 "'Vema, inaonekana kwangu, kana kwamba, kama umejenga safina na umefanya sehemu yako, Mungu atafanya sehemu Yake.'

106 "Atafanya, bali hakusema ni lini atakapofanya hivyo. Alisema tu itafanya hivyo. 'Itanyesha.'"

107 Kwa hiyo tunaona, yeye alisema basi, "Miaka ikapita, mpaka miaka mia moja na kumi na tisa, zikisalia tu yapata siku saba ifike miaka mia moja na ishirini. Bw. Kutokuamini, Bw. Mwenye Kudhihaki, hawa wengine wote, Bw. Mwenye Kushuku, hasa, na Bw. Mkosa Subira, wote walinidhihaki, na kila kitu, na kusema nilikuwa 'Mwendawazimu, kuamini ahadi ya kijinga kama hiyo. Kwamba, kama Mungu aliniahidi hilo, Yeye alisema kitu ambacho kilikuwa si kweli, wala hakuweza kutimiza kile alichosema.' Lakini nilimwamini Mungu, na kushikilia imara. Haya basi, nilimwamini. Nilishikilia imara.

108 "Na, wajua, siku moja walikuja kunicheka, ndipo mlango ukafungwa. Wakasema, 'Vema, maskini mzee mlokole alienda kule nje na kuufunga mlango, nadhani.' Ila niliwasikia. Lakini nikawaambia, 'Mungu aliufunga mlango. Hapana shaka mvua itanyesha leo hii! Hivyo ndivyo itakavyokuwa.'

109 "Siku ya kwanza ikapita, hamna mvua, basi wakanidhihaki kwelikweli. 'Kusema, "Mungu aliufunga mlango." Siamini upuuzi kama huo. Nuhu aliufunga mlango, mwenyewe, yeye pamoja na wanawe.' Mnaona, Mwenye Kudhihaki, Asiyeamini, Mwenye Kushuku!

110 "Vema, iliendelea kitambo kidogo, bali tarehe kumi na saba Mei, asubuhi moja, ikanyesha. Nayo—nayo kabisa iliangamiza hao wote waliokuwa wamewekwa kwenye jaribio dhidi ya Neno la Mungu, na kuwaokoa wale waliomwamini Mungu na kufanya maandalizi kwa ajili yake."

Nuhu akasema, "Hebu nishuhu-. . . "

111 "La, Nuhu, shuka chini. Hebu tumwite shahidi mwingine. Hatuna wakati alasiri ya leo."

112 "Hebu tumwache sha—shahidi wa utetezi sasa amwite shahidi wa pili. Atamwita Ibrahimu.

113 Ibrahimu akasema, "Nilikuwa tu mtu wa kawaida, mwaminio, ndipo Mungu akanena nami kwa Neno Lake, na kusema, siku moja, kwamba 'ningempata mtoto, kwa Sara.' Sara alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, nami nilikuwa na sabini na mitano. Nilimwoa alipokuwa na yapata umri wa miaka kumi na sita. Alikuwa dada yangu wa kambo. Naye alikuwa ni mgumba, nami vivyo hivyo. Alikuwa ni tasa,

nami nilikuwa mgumba, kwa hiyo hapakuwapo na njia kwetu kumpata mtoto huyu. Na kwa hiyo tukaendelea, kwa miaka. Lakini Mungu aliahidi, nasi tukashuka tukaenda na kununua nguo za madoadoa zote na pini, na kila kitu, tukajiandaa kwa ajili ya mtoto huyo mchanga, na kutengeneza vijibuti vidogo. Ndipo Sara . . .

114 "Basi mwezi wa kwanza ukapita, nikasema, 'Sara?' Kumbukeni, amefunga hedhi kwa karibu miaka ishirini. Mnaona? Basi akasema, 'Sasa, Sara, kuna tofauti yoyote siku hizi—siku hizi ishirini na nane?'

"'La, hakuna tofauti.'

115 "Vema, nilijua tutampata mtoto huyo, kwa vyovyote vile. Ndipo tukaendelea na kuendelea, mwaka baada ya mwaka, nami ningali nilimwamini Mungu.

116 "Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira, walijaribu walivyoweza kupata njia. Walijaribu kuniambia nilikuwa nimekosea. 'Mbona, Ibrahimu, ulikuwa mkulima aliyefanikiwa, ulikuwa mtu mzuri, kila mtu alikuwazia, ila umepotea kwa kwenda zaidi upande huo mwingine. Unaamini jambo lisiloweza kuwa kweli. Kisayansi haiwezekani mzee kama wewe, na mwanamke mkongwe kama Sara, kuzaa mtoto.'

117 "Lakini nilimwamini Mungu, haidhuru! Ilikuwa ni miaka ishirini na mitano baadaye. Hakuniambia ni lini nitampata mtoto huyo, ila alisema nitampata. Nami nikamwamini Mungu, na kuhesabu chochote kilichokuwa kinyume kana kwamba hakikuwako."

118 "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini. Haidhuru ni wenye kudhihaki wangapi waliosema, 'Sivyo! Huwezi! Haiwezekani! Jirudie! Una kichaa!' Alisema alizidi kupata nguvu, wakati wote." Hivyo ndivyo imani halisi ifanyavyo. Haijui shaka lolote. Lakini kama hujui hilo, utakata tamaa upesi sana.

119 "Kwa hiyo, vema, Ibrahimu, na—nafikiri unge—ungekuwa shahidi mzuri sana."

120 "Neno halikusema ni lini nitakapopata mtoto, mwezi wa kwanza, bali lilisema tutapata mtoto."

121 Vema, hebu tumwite shahidi mwingine upesi sana. Isaya, nabii, hebu tumwulize jambo fulani.

122 "Mbona," akasema, "Bwana alinena nami siku moja, katika unabii. Nilikuwa na—nabii. Kila mtu alijua ya kwamba kile nilichosema, Bwana alikiheshimu, nao wote waliniamini kama nabii. Ndipo siku moja kukatokea kitu cha kijinga, Nacho kikasema, 'Bikira atachukua mimba.' Vema, sasa, hilo lilikuwa lisilo la kawaida."

123 Na kwa kawaida ni katika kitu hicho kisicho cha kawaida ambamo Mungu hutenda kazi. Mnaona, ni la kigeni sana. Kama vile Yusufu, a—alitaka kumwamini Mariamu, bali lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida sana, mnaona, lisilo la kawaida sana.

124 Kwa hiyo akasema, "Wakati nilipotoa unabii huo, kila mtu aliniamini. Kwa hiyo kila msichana mdogo akajiandaa, ambaye hakuwa ameolewa, akajiandaa ku—kumzaa Mtoto wa kibikira. Siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, ukapita, ndipo basi wakaanza kuamini ya kwamba nilikuwa nabii wa uongo. Lakini nilijua ilikuwa ni Mungu yeye yule ambaye daima alikuwa ametoa ahadi hizi, kwa hiyo nikadumu moja kwa moja nayo. Basi ilikuwa ni miaka mia nane baadaye, kabla mtoto hajaja, bali bikira kweli alichukua mimba. Maneno Yake yakatimia."

125 Upesi, hebu tumwite shahidi mwingine. Hebu tumwite Musa. "Musa, ulizaliwa . . . "

126 Manabii wote wamechaguliwa tangu zamani, tunajua hilo. "Karama na miito, havina majuto." "Yeremia," Mungu alisema, "kabla hata hujaumbwa katika tumbo la mama yako, nalikujua na kukutakasa, na kukuweka kuwa nabii wa mataifa." Yesu Kristo alikuwa yule "uzao" wa mwanamke, kutoka bustani ya Edeni. Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, Isaya alimwona, kasema, "Yeye ni sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Itengenezeni njia ya Bwana.'" Mnaona, karama na miito siyo kuwekeana mikono. Ni kile Mungu afanyacho. Kuzaliwa, tangu kuzaliwa, mnaona, karama hizo zimo moja kwa moja ndani yako unapozaliwa. Angalieni.

127 Musa, aliyezaliwa kuwa nabii. Naye huyu hapa huko nyikani, baada ya miaka arobaini ya ku—kuondosha elimu yake aliyopata huko Misri. Na hata hivyo Mungu alimtokea, na kunena kwa ishara, na katika sauti; Nguzo ya Moto, na sauti iliyokuwa ya Kimaandiko sana. "Na kusema hivi, 'Niko pamoja nawe, Musa. Utakuwa kinywa Changu.'" Ndipo Musa akasema, "Nikalalamika. Si—sikudhani kinywa changu kilistahili. 'Ki—kidogo mimi hugugumiza. Usemi wa—wa—wangu si mzuri.' Basi Mungu akaniambia, 'Ni nani aliyekiumba kinywa cha mwanadamu? Na, kama huwezi kuamini hilo, ninajua Aaroni anaweza kuzungumza vizuri, ndugu yako. Wewe uwe ni Mungu, naye acha awe nabii wako; acha ayatekeleze mambo, nawe useme Neno. Nami nitakuwa kinywani mwako na kunena Neno.' Sasa, huo ni mpangilio mzuri sana, kwa hiyo nikaenda.

128 "Basi kila mtu alinicheka, kwa kuwa nilikuwa wakati huo na umri wa miaka themanini. Nilikuwa na ndevu nyeupe zimening'inia huku chini kabisa namna *hii*. Naye mke wangu alikuwa ameketi juu ya nyumbu, na maskini mtoto Gerishomu ubavuni mwake, nami nilikuwa nimeshika njia kwenda Misri. Nayo macho yangu yalikuwa yameelekezwa Mbinguni, na maskini fimbo hii iliyopinda mkononi mwangu. Nilikuwa

nikishuka kwenda kuiteka; uvamizi wa mtu mmoja." Na ukweli ni kwamba, yeye aliiteka. Hiyo ni kweli. Alifanya hivyo kwa fimbo iliyopindika, ambapo asingeweza kufanya hivyo kwa jeshi. Lakini, Mungu alisema hivyo, hilo latosha.

129 "Kwa hiyo wakati nilipokuja mbele za baba mtakatifu Farao kwa mara ya kwanza, mchungaji, mwajua, na kufanya mwujiza ambao Mungu aliniambia nifanye; ishara kwa mkono wangu, ama kwa kijiti; mwajua, mchungaji Farao, huko chini, kwanza kabisa, hakutaka kushirikiana nami. Lakini iliponibidi kulazimisha njia yangu, kuipata, mwajua, kwa namna fulani alifanya, alijaribu kuifanya kazi ya Bwana kuonekana ya kidanganyifu. Alisema alikuwa na wachawi pale ambao wangeweza kufanya jambo lile lile. Ndipo waigaji wa kimwili wakainuka kuigiza."

130 Hivyo ndivyo hasa Shetani anavyofanya katika kila hatua. Mwigaji wa kimwili; mtu anaona kitu kikifanywa, na mtu mwingine anajaribu kukiiga.

131 "Wakati hao waigaji wa kimwili walipoinuka, na kuzigeuza fimbo hizo kuwa nyoka, kama tu vile nilivyofanya, mchungaji Farao alisema, 'Unaona, si kitu ila mchawi, mchawi wa pesa nane. Nasi tuna jambo lile lile hapa, na la kisayansi, kadhalika. Sisi, wewe, tulifanya tu vile vile hasa. Tunazo hospitali na kadhalika sasa.' Hakika, ninaamini hivyo, bali hivyo sivyo Mungu alivyosema. Mnaona?"

132 Sasa yeye akasema, "Angalia," kasema, "sisi . . . alijaribu kulifanya lionekane la kidanganyifu, upande wangu. Lakini nilikuwa na hakika, nilijua ile sauti iliyosema nami ilikuwa ni Neno la Mungu lililoandikwa na kunenwa kwa ajili ya enzi hii. Kwa hiyo nilishikilia tu imara, Naye akawasukumia mbali nami. Hatimaye akatuleta kwenye mlima ambapo aliniambia. Baada ya muda mrefu, mrefu sana; sio siku hiyo, bali muda mrefu baadaye, hatimaye tulifika kwenye mlima ambapo Yeye alisema, 'kwa ajili ya ishara' ningerudi 'kwenye mlima huu.' Nilishikilia imara."

133 Hebu tumnyakue shahidi mwingine upesi, upesi sana, kabla hatujaondoka. Hebu tumvute Yoshua hapa.

134 Yoshua alisema, "Musa alimchukua mmoja kutoka katika kila kabila, kila dhehebu, kisha akatutuma kule kuipeleleza nchi. Basi tulipofika kule mtoni, na kuangalia ng'ambo ya pili tukawaona hao Waamaleki, na Waamori, Waperezi, na kadhalika, kasema, hao walikuwa ni majitu." Kasema, "Watu wakapaza sauti, kwa hofu, 'Vema, hatuwezi kufanya hivyo! Kama tukiwahi kuudhamini mkutano kama huo, shirika letu litatufukuza. Kamwe hatuwezi kufanya hivyo. Ha—hatuwezi kuwa na mambo kama hayo. Ni ya kidanganyifu sana, mnaona. Hatuwezi kamwe. Mbona, haiwezekani.' Ndipo waliporudi,

ingawa walikuwa na ushahidi, walirudi na zabibu kutoka kwenye nchi hiyo."

135 Basi, shida yake ni kwamba, mtu anawezaje, ama kanisa, ama dhehebu, lililopata kuonja ushuhuda kwamba Yeye yu hai, kisha amkane wakati amefufuka miongoni mwetu? Mnawezaje kufanya hivyo, enyi Wapentekoste? Mmenena kwa lugha na kuzifasiri lugha, kama mnavyodai, basi mnawezaje kulikataa Neno lenyewe lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huu? Mnachukua sehemu Yake, na kusema, "Ni Nchi nzuri. Hatukujua!" Ilikuwa ni Nchi nzuri. Imethibitika kuwa ni Nchi nzuri, lakini shada hilo moja la zabibu halikuwa ndilo lote. Palestina nzima ilikuwa imejaa hizo! Tunaamini katika kunena kwa lugha, na miujiza hii mingine yote na kadhalika, na kuwaombea wagonjwa.

136 Ndipo wakati ahadi inapofikia hapa juu, kwenye kitu kingine, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Malaki 4 ilisema, "Kabla tu ya ule wakati mkuu ambapo ulimwengu wa Kimataifa utateketea kama tu vile Sodoma ilivyoteketezwa, halafu wenye haki watetembea juu ya waovu, nitawapelekea Eliya aliyetiwa upako na Roho, naye ataigeuza mioyo ya watoto iielekee Imani ya baba zao." "Kurejeshwa," daima, kila moja ya nyakati alizokuja, hivyo ndivyo ilivyokuwa.

137 Basi mwawezaje kushuku hilo, wakati Yeye anapomleta Kristo, ahadi, manabii, Neno, na kila kitu, na kukitambulisha kikamilifu; kisha mgeuke na kusema, "La, msishirikiane na mkutano huo. Mkishirikiana, nitawapa makaratasi yenu"?

138 Ingekuwa ni sehemu yangu, wangeweza kupata ngozi zao za mbuzi! Jina langu limeandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, na kila mwaminio. Kwa hiyo wakarudi, ndipo Yoshua akasema, "Wakati wote walipokuja . . ." Ningeweza kukaa pale muda mrefu, bali nina hakika mnajua yale ninayozungumzia.

139 Kwa hiyo Yoshua akasema, "Nikawatuliza watu. Kasema, 'Sijali jinsi wanavyoonekana wakubwa, kuna upinzani kiasi gani, jinsi inavyoonekana ya kilokole! Kumbukeni, Mungu alisema, tulipokuwa huko Misri, "Nimewapa nchi hii. Ninawapa ninyi."'"

140 Sasa yeye haingii tu mle ndani, aifagie na kuzikandika kuta, kisha akwambie uingie na kuchukua kiti cha Morris na kuketi chini, aseme, "Tutakuwa na wajakazi wa kukutandikia kitanda." Yeye halifanyi hivyo. Huna budi . . . Yoshua aliambiwa na Mungu, "Kila mahali nyayo za miguu yako zitakapokanyaga, hapo nimewapa ninyi." Nyayo za miguu zilimaanisha umilikaji. Na kila ahadi kwenye Kitabu hiki ni ya waaminio, bali huna budi kutia nyayo za miguu Mle. Huna budi kupigania kila inchi ya njia hiyo. Usipokuwa na uwezo wowote wa kupigana ndani yako, basi ondoka kwenye mchuano.

141 Niliingia hapa ndani, sio muda mrefu uliopita, ninaamini ilikuwa ni kwenye mkoa huu. Georgia Tech, ama mahali fulani kule juu, nilikuwa na ninii . . . Sijui—sijui sasa, huenda ilikuwa ni huko Mashariki. Niliingia kwenye uwanja wa kandanda, nikaona kibao ki—kidogo ambacho kwa namna fulani daima kilinivuvia. Kulikuwako na kibao juu ya mlango, nilipotoka kwenye vyumba vya kuvalia nguo. Mle ndani mlikuwamo na kibao, kikasema, "Sio ukubwa wa mbwa katika pambano, ni ukubwa wa pambano ulio katika mbwa." Na hiyo ni kweli.

142 Si—si kwamba una D.D.D., Ph. D., LL.D. ngapi. Ni kiasi cha Kristo kilicho ndani yako. Inategemea kuna kiasi gani cha imani mle, sio jinsi unavyoweza kuelezea *hili* na kuelezea *lile*, na kulielezea Hili vinginevyo. Ni kwamba una kiasi gani cha imani katika Mungu, kuamini ya kwamba Yeye husema Kweli. Vema, hiyo ni juu yako. Inategemea wewe ni wa ukoo gani. Iwapo wewe ni Uzao wa Ibrahimu, utafanya kama Ibrahimu afanyavyo, "Kuyaita mambo, ambayo hayakuwako, kana kwamba yapo."

143 Sasa Yoshua alisema, "Niliwatuliza watu, kwa kuwaambia, 'Nyamazeni! Mungu alisema hivyo!'" "Mungu alisema hivyo, hiyo ni kweli. Lakini, mwajua, walikuwa tu siku mbili kutoka huko. Huko ni Kadeshi-Barnea. Walikuwa tu siku mbili, wangalikuwa kwenye nchi ya ahadi."

144 Lakini Yoshua alisema, "Ilitimia miaka arobaini kabla hatujaiteka nchi hiyo. Hakusema ni lini tungeiteka nchi hiyo. Lakini alisema alikiacha kizazi hicho cha kale kife, hao wasioamini, kisha akainua kizazi kingine kilichoamini. Hakusema wangeiteka nchi lini. Lakini alisema wangeiteka nchi, nasi tukaiteka!" Nafikiri yeye ni shahidi mzuri. Mwaonaje ninyi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika. "Tuliiteka nchi hiyo, baada ya miaka mingi sana."

145 Sasa tunachelewa. Sasa hebu nimchukue tu shahidi mwingine mmoja. Je, tunaweza? Ninao dazani moja wameorodheshwa hapa chini. Tungewaita mia moja, ama mia mbili, lakini hebu nimwite tu mmoja zaidi. Na kama mtaniruhusu, naweza kuwa shahidi huyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ningetaka kusimama kizimbani kumtetea. Hizo siku ziko huko nyuma; hii ni hapa sasa. Ninajua huo ungekuwa ushuhuda wao, bali hebu nisimame kwenye kizimba cha kushuhudia mara moja. Loo, jamani!

146 Ninakumbuka huko chini, nilipokuwa mvulana mdogo. Mmeisoma hadithi ya maisha yangu, na mnaijua hadithi hiyo. Ninakumbuka, kule chini mtoni, nilipokuwa kijana mhubiri wa Kibaptisti, na nilikuwa nikibatiza huko. Karibu watu elfu kumi wamesimama ufukoni, wakati alasiri moja . . . Uamsho wangu mkubwa wa kwanza, waongofu karibu elfu moja, nami nilikuwa nikiwabatiza huko nje majini. Mtu wa kumi na saba, nilikuwa nikimwongoza huko majini. Nikasikia sauti, nami nikaangalia

kila mahali. Kulikuwa na joto. Ilikuwa ni Juni, 1933, mwanzoni mwa Barabara ya Spring huko Jeffersonville, Indiana. Nilikuwa nikiwaongoza kule. Nazo fuko, kote huku na huku, kulijaa watu.

147 Nilitoka na maskini mvulana huyu. Nilikuwa nimemwona madhabahuni. Nikasema, "Mwanangu, hivi umemkubali Yesu Kristo kuwa Mwokozi wako binafsi?"

Akasema, "Nimemkubali."

148 Jina lake lilikuwa ni Edward Colvin. Nami nikasema, "Edward, je! unajua ninalofanya sasa?"

Akasema, "Ninajua, Ndugu Branham."

149 Nikasema, "Ninakubatiza, nikiionyesha hadhara hii huku nje, ya kwamba umemkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi. Nitakapokubatiza katika Jina la Yesu Kristo, utalichukua Jina Lake. Utafufuka kwenye maisha mapya. Basi utakapoondoka hapa, unapaswa kutembea maisha mapya. Unaelewa hilo, Edward?"

Akasema, "Ninaelewa."

Nikasema, "Inamisha kichwa chako."

150 Nikasema, "Baba wa Mbinguni, kwa kuwa mvulana huyu amekiri imani yake Kwako. Na kama vile Wewe umetuagiza 'enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,' tukiwaagiza kuamini mambo yote ambayo umefundisha."

151 "Kwa hiyo ninakubatiza, ndugu yangu mpendwa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo."

152 Basi nilipokuwa nikimzamisha majini, nikainuka, nikasikia kitu kikienda, "Huuush!" Nikauangalia umati, na ikaninii . . . Nikasikia Sauti ikisema, "Angalia juu!"

153 Nikawaza, "Ni kitu gani hicho?" Billy hapa, mama yake, miaka miwili ama mitatu kabla hatujafunga ndoa, alikuwa amesimama pale. Niliuona uso wake, mweupe. Alikuwa ameshika kamera mkononi.

154 "Angalia juu!" Nikaisikia mara ya pili. Niliogopa. Nikaangalia kila mahali, watu wamesimama pale wakiangalia tu, wameduwaa kabisa. Nikaisikia ikisema tena, "Angalia juu!"

155 Ndipo nilipoangalia, hii hapa ikaja Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza Israeli nyikani. Maelfu ya macho yakiiangalia ikishuka moja kwa moja mahali nilipokuwa nimesimama. Ndipo ikasema, "Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kukutangulia kuja mara ya kwanza kwa Kristo, Ujumbe wako utaenea duniani na kukutangulia Kuja kwa Kristo Mara ya Pili."

156 Hayo yaliingia kwenye gazeti, kwenye Shirika la Waandishi wa Habari. Daktari Lee Vayle, hapa alasiri ya leo, alilichukua, huko mbali Kanada na kote kote, "Mhubiri wa kawaida wa

Kibaptisti, wakati akibatiza, Nuru isiyo ya kawaida inaonekana juu yake."

157 Moja kwa moja kule Dallas, Texas, ama Houston, Texas, miaka michache iliyopita. Wakati watu walipoishuku, na ilikuwa ni vigumu kwangu kujua la kufanya. Wakati mhubiri mwerevu wa Kibaptisti alipotaka kufanya mjadala na Ndugu Bosworth, "Hakukuwako na kitu kama uponyaji wa Kiungu." Basi aliposhindwa mjadala, kwa asilimia mia moja, alisema, "Hebu nimwone huyu mponyaji wa Kiungu akija huku na kutenda!" Nikasema . . .

158 Nikashuka. Nilikuwa kwenye roshani. Nikasema, "Mimi si mponyaji wa Kiungu, bwana."

159 Nikasema, "Usingetaka kuitwa 'Mwokozi wa Kiungu.'" Nikasema, "Bw. Bosworth amekuuliza swali hili: 'Je! majina ya ukombozi ya Yehova yalitumika kwa Yesu, ndio ama la?'" Wala huwezi kumjibu. Swali moja tu, hivyo tu. Ikiwa Yeye ni Yehova-Yire, hana budi kuwa; ikiwa siye, Yeye si Mwokozi. Wala huwezi kuyatenganisha majina hayo. Yeye ni Yehova-Rafa, mponyaji! 'Yeye yule jana, leo, na hata milele!'"

160 Mtu huyo asingeweza kusogea, ila alisimama hapo na kugugumiza maneno. Na wengi wenu mlikuwa kule, nadhani, kusikia hayo. Kwa hiyo Bosworth akawa ndiye mshindi wa mjadala huo. Wala hata hakupata pointi moja, ndipo wakati ilipokuwa . . . Huo ulikuwa umeandaliwa na maafisa wa jiji, ambao hawakuwa na upendeleo, ni kujua tu vile Maandiko yalivyosema.

Basi akaendelea tu kusema, "Hebu na ajitokeze."

161 Hawakujua nilikuwa kule juu. Nami nilikuwa nimeketi kule juu pamoja na mke wangu na mtoto Becky. Anahitimu kutoka shule ya sekondari mwaka huu. Nami nilikuwa nimeketi pale, naye alikuwa na umri wa mwaka mmoja tu. Nilikuwa nimemshika mikononi mwangu.

162 Ndipo akasema, Ndugu Bosworth akasema, "Ninajua Ndugu Branham yuko mkutanoni. Akitaka kuja na kuufunga, vema." Lakini nikasema mimi . . . Basi kila mtu akaanza kuangalia kila mahali.

163 Basi pale walisimama kama mamia mengi ya watu, maelfu, karibu watu elfu thelathini. Tulikuwa tukiwa na mia nane, kila wakati, huko kwenye nyumba ya muziki. Na, huu, watu walikuja kwa ndege, kwa garimoshi, na kila . . .

164 Na hapo ndipo nilipojua; makundi yote ya Kipentekoste yalikutana wakati huo. Itahitaji mateso, kuwaleta enyi watu pamoja. Kamwe hamtaamini, ila hapo wakati huo utakapotimia . . .

165 Mnaona, jambo moja waliloamini pamoja, uponyaji wa Kiungu, kwa hiyo Wa-umoja, Wa-uwili, Wa-utatu, Wa-unne, na wowote wale, wote walikuja pamoja. Nao hao hapo.

166 Basi mtu huyu akasema, "Hakuna mtu anayeamini uponyaji wa Kiungu ila kundi la watakatifu wanaojifingirisha."

167 Raymond Richey akasimama, kasema, "Unaowazia kuwa watakatifu wanaojifingirisha ni nani?" Kasema, "Ni kina nani ungewahesabu kuwa ni wenye akili timamu?"

Akasema, "Baptisti."

168 Akasema, "Vema. Ni wangapi walio humu jengoni sasa, wanaoweza kuonyesha kwa cheti cha daktari ya kwamba Yesu Kristo alikuponya wakati Ndugu Branham alipokuwa hapa?" Ndipo mia tatu wakasimama. Kasema, "Vipi kuhusu hao?" Mnaona? Kwa hiyo akapiga tu vita kwa hasira.

169 Nilidhani nitashuka chini. Nilimsikia Roho Mtakatifu akisema, "Shuka chini." Nikaangalia, na hapa kulikuwako na Mwanga huu ulioning'inia papo hapo juu ya mahali nilipokuwa. Nikateremka kule.

170 Nikasema, "Ikiwa ile karama inashukiwa, hilo ni jambo lingine. Lakini mimi si mponyaji. Mungu Ndiye mponyaji." Ndipo nikasema, "Kama nikimshuhudia Mungu, Mungu anawajibika kunishuhudia."

171 Sasa, Studio za Daouglas, zikiwa na kamera kubwa iliyowekwa pale. Wakasema, mhudumu huyu akasema, "Piga picha kwa flashi za mzee huyo; nitamchuna kisha nimchune ngozi yote, na kuibandika ngozi yake kwenye mlango wa chumba changu cha kusomea, kama kumbukumbu ya uponyaji wa Kiungu." Ungeweza kuwazia Mkristo akisema hivyo juu ya Mkristo mwenzake? Mnaona, unatambulikana kwa tunda lako. Kwa hiyo, basi akapiga picha sita kwa flashi. Ndipo akaweka ngumi yake chini ya pua ya Ndugu Bosworth, kabla hawajaanza mjadala, akasema, "Ipige *hivi*," naye akaipiga. Ndugu Bosworth alisimama tu pale.

172 Nanyi mwajua nini? Wakati alipozipeleka hizo kwenye studio kule nyuma, zikachunguzwe, hakukuwako na hata moja yazo. Kila moja yazo ilikuwa imefutiliwa mbali. Mungu asingemruhusu kafiri huyo kuweka kidole chake chini ya pua ya mtauwa, namna hiyo, akazipiga picha hizo.

173 Basi wakati nilipokuwa nimesimama pale, nilisema, "Kama ni swali juu ya karama ya Mungu, ya utambuzi, hiyo ni Maandiko yaliyoahidiwa. Hilo linaweza likathibitishwa. Hilo linaweza likathibitishwa." Ila nikasema, "Kuhusu mimi kuwa mponyaji, la, bwana, mimi si mponyaji, bwana."

174 Akasema, "Kama mwanadamu, ninakuheshimu. Kama mhudumu, na—nakudharau."

175 Nikasema, "Natoa shukrani zangu," na kwa hiyo tukaendelea tu namna hiyo.

176 Kwa hiyo akasema, "Ningetaka kukuona ukitenda kazi. Ningetaka kukuona ukimpumbaza mtu akili, kisha niwaone baada ya mwaka mmoja tangu leo." Akaanza kugeuka.

177 Nikasema, "Kama nikizungumza kwa niaba ya Mungu, Mungu anawajibika kuzungumza kwa niaba yangu." Kabla sijamaliza kusema hilo, hiki hapa hicho kisulisuli kinakuja tena. Papo hapo hadharani ambapo kilikuwa, ile Nguzo ya Moto ikashuka. Basi hiyo kamera kubwa ya studio, sasa, ikapiga picha.

178 George J. Lacy, kiongozi wa makachero wa FBI wa alama za vidole na hati, aliipiga usiku wa manane usiku huo. Walipoiweka, ndiyo ya pekee iliyokuwa na picha. Nanyi . . .

179 Ni wangapi walio nayo kwenye rafu zenu nyumbani mwenu? Mnaona? Imetundikwa huko Washington, DC, kwenye ukumbi—ukumbi wa sanaa za kidini, "Kiumbe cha pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha katika historia yote ya ulimwengu."

180 Ni kitu gani? Angalieni! Iangalieni juma hili. Angalieni vile imefanya. "Jana, leo, na hata milele, yeye yule!" Sasa, kama ningalikuwa na ndimi elfu kumi, nisingeweza kumalizia kuzungumza juu Yake. Naam, bwana.

181 Mchungaji wangu aliniambia, huko nyuma, kasema, "Jamani, uliota kwelikweli!" Haidhuru kile alichokuwa . . .

182 Nakumbuka wakati nilipoanza kutoka kwa mara ya kwanza, na kukutana nanyi watu kwenye nchi hizi. Yeye aliniambia, kasema, "Karama ya kwanza itakuwa kwamba wewe," ile Sauti iliyo nyuma ya hii, "itakuwa kwamba utaweka mikono yako juu ya wagonjwa, wala, usiseme kitu, Hiyo itasema ni kitu gani." Ni wangapi wanaokumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Naam."—Mh.] Nami nikasema . . . "Ndipo itakuwa," Yeye aliniambia usiku ule wakati aliponikuta huko kwenye Kinu cha Green, Naye . . . Nilimwuliza habari zake, Naye akasema, "Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku za mwanzoni." Kasema, "Bwana wetu, wa—walilifanya vile vile. Nayo hii ndiyo saa ambapo haya hayana budi kutimizwa."

183 Ninajua kuna ulokole mwingi sana ulimwenguni. Siwajibiki kwa shuhuda za watu wengine. Inanibidi tu kuwajibika kwa wangu. Niko kwenye kizimba cha kushuhudia, nikimtetea Mungu pamoja na Neno Lake, kwamba ninajua ni kweli. Nalo Neno Lake, nilipomsikia akiniambia jambo hilo, nisingaliamini kama asingalikuwa amenionyesha katika Biblia ya kwamba imeahidiwa kwa ajili ya siku hii.

184 Ni wangapi wanaokumbuka niliwaambia ingetimia, alisema, kwamba, "Ungejua siri za moyo wao hasa"? Inua mkono wako. Unaona? Je! ilitimia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni

miaka thelathini na mitatu baadaye. Halikutukia papo hapo. Lilifikia hapo, kama mbegu inavyokua. Lilichipuka, kama Neno Lake. Na, leo hii, mimi ni shahidi ya kwamba Yeye yu hai. Mimi ni shahidi kwamba Yeye huponya.

185 Sikilizeni. Hatuna muda mwingi uliosalia; ni wa mstari wa maombi tu.

186 Kumbukeni, nitaifunga kesi hii, na kuiacha tu namna hii. Kama . . . Unaweza kuwaamini mashahidi wowote utakao, lakini, kumbuka, moyo wako ndio wazee wako wa mahakamani. Katika kila kesi inabidi kuwe na wazee wa mahakamani. Halafu basi jinsi utakavyotenda, tangu sasa, kutatangaza uamuzi wako.

187 Sasa tutafanya jinsi tu Biblia ilivyosema, "Kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Hiyo ni, waaminio. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Sasa kama mnaamini, tunaamini; mamia hapa wangeweza kusimama, kote nchini.

188 Florence Nightingale, kilembwe cha hayati Florence Nightingale huko London, Uingereza. Akilala, mmeiona picha yake pale, kivuli kitupu. Kansa ilikuwa imemla kabisa. Mmeiona picha yake kwenye ukurasa unaofuata?

189 Mwangalieni Mbunge Upshaw, kwenye kiti cha magurudumu, miaka sitini na sita. Alisimama kule Kalifornia usiku huo. Nami nikaingia, nikaenda jukwaani, nilikuwa nimesimama pale. Nao wakaanzisha mstari wa maombi.

190 Nikasema, "Ninaona mama mwe—mwe—mwe—mweusi hapa mbele yangu, naye ana maskini mtoto mchanga. Kuna daktari amesimama, ambaye—ambaye amemfanyia mtoto huyo upasuaji naye amempoozesha. Huyo daktari alikuwa mwembamba. Alikuwa amevaa miwani ya kobe. Nao ulimpoozesha mtoto huyo."

191 Huko mbali sana upande wa nje kule, maskini shangazi Jemima wa kawaida mwenye uzito wa karibu ratili mia mbili na hamsini, huyu hapa anakuja, akiwasukuma mabawabu pande zote, akivuta machela yaliyombeba mtoto wake mchanga. Kasema, "Bwana, rehemu, huyo alikuwa ni mtoto wangu mchanga."

192 Naye bawabu akasema, "Huwezi kuingia mstarini, huna kadi ya maombi, mama." Vema, nikasema, "Mama . . . "

193 Akasema, "Mimi anapanda kule juu." Wala wasingeweza kumzuia. Alikuwa mnene sana kwao, kwa hiyo alikuwa akijisukumiza moja kwa moja mstarini. Akapanda juu.

194 Basi alipofika pale, karibu sana na pale, nikasema, "Hebu kidogo, mama. Kama Bwana Mungu angeweza kujua kile kilichokuleta kule . . . " Nikasema, "Huyo ndiye yule mtoto, vema." Nikasema, "Siwezi kukwambia lolote juu yake." Nikasema, "Jambo pekee nijualo ni kumwombea tu mtoto, nami

nitafanya hivyo kutoka papa hapa." Nikasema, "Ila jambo pekee ninaloweza kusema ni kile nilichoona."

195 Akasema, "Hiyo ilikuwa ni karibu miaka miwili iliyopita, bwana." Naye akasema, "Mtoto wangu, wakati walipotoa mafindo, ilimpoozesha mtoto." Kisha kasema, "Amepooza tangu wakati huo."

196 Nikasema, "Vema, kama imani yako ingeweza kumgusa, kushusha hilo, mbona usiketi tu pale na kuomba?"

197 Nikageuka. Nikasema, "Kama nilivyokuwa nikisema, katika ujumbe wangu . . ." Nami nikaangalia, na nikaona msichana mdogo mweusi, yule yule, akienda zake mtaani, ilionekana kama ni kichochoro, huku ameshika mwanasesere mkononi mwake, anaenda akimpembeza.

198 Nikasema, "Shangazi, Mungu ameyasikia maombi yako. Mtoto huyo ameponywa." Mtoto akasimama. Nami ilinibidi kumnyamazisha, kwa kitu kama wanamgambo, na kumshusha mtoto huyo kupitia kwenye umati kama huo.

199 Dakika chache tu, nikasema, "Ninamwona mzee. Yuko kwenye lundo la nyasi kavu, sasa yeye ni mvulana mdogo, alianguka akaumiza mgongo wake." Nikasema, "Iliwabidi kuchimba mashimo sakafuni machela yake isije ikatikisika sakafuni." Kundi la waaminio, kila mtu katika moyo mmoja na nia moja, wameketi, mamia mara mamia. Kisha nikasema, "Amekuwa mtu mashuhuri, msemaji wa namna fulani." Ndipo likaniacha. Nami nikaendelea, nikaanza.

200 Papo hapo, Daktari Ern Baxter akakuta, huko nyuma kabisa kwenye kiti cha magurudumu, kundi moja huko nyuma kabisa. Akasema, "Huyo alikuwa ni Mbunge Upshaw. Ulipata kusikia habari zake?"

Nikasema, "La, bwana."

Akasema, "Miaka mingi iliyopita, yeye aligombea Urais."

Nikasema, "Simjui, bwana," nikasema.

Akasema, kasema, "Kama nitamleta, kuonyesha?"

Basi nikasema, "Yeye ni nani?"

Kasema, "Ameketi pale pale."

201 Na kwa hiyo wakamsukuma kwa kiti cha magurudumu, mke wake alimsukuma. Akasema, "Kijana, uliwezaje kunijua?" Kasema, "Daktari Roy E. Davis, yule aliyekuweka wakfu katika kanisa la Kimishenari la Baptisti, na—naye alikuwa m—msemaji mkuu wa Kongamano la Baptisti ya Kusini," akasema, "yeye ndiye aliyenituma hapa ukaniombee." Kasema, "Nimeombewa, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, bali daima nimeamini kwamba Mungu ataniponya, maana nilichukua msimamo wa haki katika wakati wa kupigwa marufuku. Mimi, wakati pombe ilikuwa iletwe, niliitwa mmoja wa mifupa mikavu." Akasema,

"Nilipoteza urais wa Marekani kwa sababu ya msimamo wangu."

202 Nikasema, "Hilo ni jambo la kishujaa, bwana." Nikasema, "Bwana na akubariki."

203 Nikasema, "Vema, mleteni mgonjwa wenu wa kwanza hapa, mtu wa kwanza atakayekuja huku." Ilipotendeka, jambo fulani likatukia kwa mama huyo, Naye akamwambia kulihusu.

204 Basi nikageuka, kuangalia tena. Nikamwona maskini Mbunge huyo mzee amevaa suti yenye milia ya pini, tai nyekundu, akiinama, akijiinamisha *hivi*, kwa watu, akitembea moja kwa moja katikati ya watu.

205 Nikasema, "Mbunge, Yesu Kristo amekuheshimu. Una umri wa miaka themanini na sita sasa, lakini Mungu amekuheshimu. Ilionekana kama, wakati alipokuwa akitaka kukuponya, angekuponya wakati ulipokuwa mvulana. Na mifupa yako ni miepesi kabisa kuvunjika mle ndani, ama ninii yote . . . Unajua, yenye kupindika, na kadhalika." Nikasema, "Inaonekana kana kwamba angalikuponya wakati huo, bali amekuponya sasa."

Akasema, "Unataka kusema nimeponywa sasa?"

206 Nikasema, "BWANA ASEMA HIVI." Nikasema, "Je! una suti yenye milia ya pini?" A—alikuwa amevaa suti nyeusi, na tai nyekundu. Nikasema, "Je! una suti yenye milia ya pini?"

Kasema, "Naam, bwana, ndio kwanza niinunue moja hivi majuzi."

Nikasema, "Simama. Yesu Kristo amekuponya."

207 Basi ni wangapi wanaoujua huo, ushuhuda wake? Alisimama kwenye mkutano wa Billy Graham, kwenye vipandio vya Ikulu, na kuimba *Kuegemea Kwenye Mkono wa Milele*. Kamwe hakurudi kwenye magongo wala viti vya magurudumu tena, wakati akiwa hai.

208 Mimi na Jack Moore tulikuwa huko chini katika Old Meksiko, usiku ule wakati iliponibidi kuteremshiwa ukutani. Maskini mwanamke mmoja pale, maskini, Mmeksiko Mkatoliki. Usiku mmoja kabla ya hapo, nilimwekea mikono maskini mzee mmoja kipofu, akapata kuona. Ndipo maskini mwanamke huyu, walisema . . . Billy alinijia, kasema, "Baba, . . . " Nilimwita mtu huyo, "Mañana." *Mañana* linamaanisha "kesho," alikuwa ni mwenda pole sana. Alikuwa akisambaza kadi za maombi; naye Billy akaambatana naye, asije akauza moja.

209 Kwa hiyo akasema alisambaza kadi zote za maombi. Kisha kasema, "Mwanamke fulani ana mtoto aliyekufa asubuhi ya leo."

210 Ilikuwa ni karibu saa nne usiku. Nje, kwenye uwanja wa mchezo wa ng'ombe pale, nayo—nayo mvua inanyesha tu, namna fulani ya uwanja mkubwa wazi. Ndipo akasema . . .

Wakaniingiza, na kuniteremshia kwenye vipandio vya kitu kama ngazi. Ndugu Jack Moore na hao wengine wako hapa sasa. Alikuwa jukwaani.

211 Kasema, "Nina mabawabu mia tatu wamesimama pale, wala hawawezi kumshikilia mwanamke huyo." Kasema, "Atapanda juu ya mabega yao, akakimbilia katikati ya miguu yao. Nami nilimwambia asingeweza kupanda huku, kwa kuwa hakuwa na kadi ya maombi. Wala hatuna kadi zingine za maombi." Hakujali hilo. Alitaka mikono iwekwe juu ya mtoto huyo.

212 Alimwona mwanamume Mkatoliki, aliyekuwa kipofu kwa muda wa miaka ishirini ama thelathini, akipokea kuona kwake kwa kuombewa. Yeye . . . na lundo la mavazi machakavu. Mnafikiri hili ni kitu? Loo, mara tatu ya jukwaa hili, yamelundikwa mpaka juu *hivi*, kwenye upeo wa macho, kukiweko na mashali machakavu na kofia. Jinsi walivyojua ni vya nani, sijui. Lakini, waliamini; imani rahisi, ya kitoto.

213 Kwa hiyo nikasema, "Vema," nikamwambia Ndugu Jack. Mimi na yeye huchana nywele zetu namna moja, mwajua, kwa hiyo ni—nikasema, "Ndugu Jack, asingejua tofauti kati yako na mimi. Shuka uende kule na kumwombea mtoto huyo."

214 Naye akasema, "Vema, Ndugu Branham." Akaanza kushuka. Sasa, Jack ameketi pale pale. Kwa hiyo tulikuwa . . . Akaanza.

215 Nikaanza kuhubiri, namna *hii*. Nami nikaangalia, ndipo nikaona mtoto mchanga, wa Kimeksiko, maskini mtoto mdogo mweusi amesimama hapa mbele zangu, akitabasamu tu, mafizi yake madogo. Hakuwa na meno yoyote. Nikasema, "Ngoja kidogo. Ngoja kidogo. Mleteni mtoto huyo hapa."

Nikasema, "Bwana Mungu, sijui."

216 Akakimbia juu, ameshika msalaba wenye sanamu mkononi mwake, akipiga makelele, "Padre," linamaanisha "baba."

Nikasema, "Simama sasa."

217 Alikuwa na maskini blanketi dogo ya bluu; na mtoto mchanga, amekauka, mfu, amelilalia; limelowa tu kwa maji, nywele zake zote chini. Maskini mama mrembo, labda ni mtoto wake wa kwanza; kwenye umri wa miaka ya ishirini, mwajua, naye alikuwa amemshika tu chini namna *hii*. Ndipo ni—nikasema, "Nitamwombea mtoto huyu." Nikamwekea mikono. Hawatafsiri maombi.

218 Nikasema, "Bwana Mungu, niliona tu ono. Sijui." Na yapata wakati huo, akatupa teke, akaanza kupaza sauti na kulia namna hiyo.

219 Nikasema, "Ndugu Espinoza," kwa mwe—mwenyekiti wa mkutano, nikasema, "usiamini tu ushuhuda wa mwanamke huyo. Mtume shahidi kwa huyo, kwa huyo daktari."

220 Daktari akatia sahihi ushuhuda unaoonekana kwenye *Sauti Ya Uponyaji* ya wafanyabiashara. "Mtoto huyo alikufa kwa nimonia maradufu, asubuhi hiyo saa tatu, ofisini mwake, ikatangazwa amekufa, hamna upumuaji; alikuwa amekaa kwenye mvua siku nzima, amekufa, kisha akaponywa." Yu hai leo, nijuavyo mimi, akiuishia Ufalme wa Mungu.

221 Ninayo mambo mengi, kutoka Afrika, ambako niliwaona makafiri watupu elfu thelathini wakiyatoa maisha yao kwa Yesu Kristo.

222 Mungu hulitimiza Neno Lake. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kama shahidi wake.

223 Wewe ni, moyo wako ndio wazee wa mahakamani. Na tendo lako ndilo hakimu wako.

Sasa inamisheni vichwa vyenu kwa muda kidogo tu.

224 Bwana Yesu, kesi haijaanza; ni wangapi zaidi tungaliweza kuwaita hapa juu jukwaani! Ulisema, "Wa—wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Ulisema, "Kazi nizifanyazo mimi ninyi nanyi mtazifanya." Yule mwanamke aliligusa vazi Lako, ukageuka na kumwambia yaliyokuwa yametukia. Nawe huyatimiza Maneno Yako yote. Hakuna hata moja lililokosea. Kosa liko ndani yake asiyeamini, Bwana. Bw. Asiyeamini, huyo ndiye anayemwambukiza mtu; Bw. Mwenye Kushuku; na yule mkosa subira asiyeweza kumngojea Bwana, na hata hivyo anajiita Uzao wa Ibrahimu. Ee Roho Mtakatifu, shahidi wa utetezi, Wewe unajua aliye na imani na asiye nayo.

225 Lakini, Mungu, ninaomba ya kwamba utaondolea mbali kila kutokuamini, alasiri ya leo. Na jalia Hakimu mkuu wa dunia nzima ajitokeze sasa, Yule aliyeliandika Neno. Yeye ni Neno. Jalia ajitokeze.

226 Basi wakati watu hawa wakipitia hapa, wapate kuponywa alasiri ya leo, jalia kila mmoja wao aamue sasa. Wako mahakamani. Ninayaweka moja kwa moja mapajani mwao, Bwana. Mioyo yao ndiyo wazee wao wa mahakamani. Na jinsi watakavyotenda tangu hapa na kuendelea, watakapopitia kwenye mstari huu, itathibitisha kile wanachowazia kuhusu Neno la Mungu.

227 Kwa hiyo tujalie, Bwana, kwamba ujumbe huu wa mwisho uliouhubiria wanafunzi Wako hapo ulipowaagiza, Maneno ya mwisho yaliyotoka kwenye midomo Yako mitakatifu, "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hao ni, waaminio. Mambo ya mwisho uliyosema. Agizo la kwanza ulilomwagiza mwanadamu kufanya, Mathayo 10, lilikuwa, "Pozeni wagonjwa, watoeni pepo, jinsi mlivyopokea bure, toeni bure." Agizo la mwisho, "Enendeni ulimwenguni kote, toeni pepo; wekeni mikono juu ya wagonjwa, watapata afya."

228 Bwana, jalia watu watambue kwamba imani hiyo hutia nanga kama ilivyofanya kwa mashahidi hawa wote. Wanaamini! Haidhuru, si lazima itendeke sasa; lakini, kile ulichosema, utakitimiza. Ulisema, "Usipotia shaka moyoni mwako, baadaye itatimia." Mbegu hiyo haina budi kukua. Jalia watu walione na kufahamu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

229 Hivi wewe ni mwaminio? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, Yeye huyatimiza Maneno Yake yote. Mnaamini hilo? ["Amina."] Sasa kwa uchaji kabisa, hebu kidogo tu kila mtu, kabla hatujaufanyiza mstari wa maombi. Tunataka utaratibu.

230 Sasa, kumbukeni, hivi mmefanya uamuzi wenu? Je! mmefikia maamuzi, enyi wazee wa mahakamani? Inueni mikono yenu kama mmefikia maamuzi. Je! Mungu ana haki ama hana haki? Je! Neno Lake . . . Je! ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ama siye? Sasa kama ukiinua mkono wako, upitie kwenye mstari huu, basi jinsi unavyotenda tangu sasa na kuendelea, je! unatenda kama Ibrahimu ama Bw. Asiyeamini? Unaona, Bw. Mwenye Kushuku, Bw. Mkosa Subira, achaneni nao! Aminini Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

231 Hatufahamiani. Lakini sasa kukufanya ujue ya kwamba Yeye angali hapa, na ikiwa tu utalikubali Neno Lake moyoni mwako.

232 Sasa huenda msiweze kufanya jambo hili. Tuna mmoja wao katika kizazi kimoja. Kulikuwako na Musa mmoja; hakuna mwingine wao aliyelazimika kuyageuza ninii . . . mavumbi kuwa viroboto, na kadhalika, na maji kuwa damu. Kulikuwako na Musa mmoja; hao wengine waliamini tu kile alichosema. Mnaona?

233 Kulikuwako na kundi pale juu lililotaka kuunda dhehebu kutoka kwake, Dathani na hao wengine. Ndipo Mungu akasema, "Jitenge nao," nao ulimwengu ukawachukua. Mnaona? Na hiyo ilikuwa ni ninii tu . . . Huo ulikuwa ni mfano, wa huu ukiwa ni uhalisia. Ulimwengu huipata, polepole. Unaona kinachompata kila mmoja wao.

234 "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, mambo yote yanawezekana, kama wakiamini. Vema, ombeni. Wekeni imani yenu juu ya Mwenyezi Mungu.

235 Kulikuwako na swali hapa nililotaka kusema hapa. Naam. Wakati jirani zako wanapokuona, na watu wanaokuona ukipitia kwenye mstari huu alasiri ya leo, wanapokuona ukipitia kwenye mstari huu, watajua uamuzi wako ni upi baada ya hapa, jinsi unavyotenda na jinsi unavyoshuhudia. Kama, mara nyingine utakapokimbia kwa mchungaji wako, "Loo, sikuupata. Ninataka kujaribu tena." Unaona, unaichimbua mbegu, haitatimia kamwe. Mnaona? Usiichimbue mbegu yako.

Ipande, kisha uiache humo. Isahau. Hiyo ni juu ya Mungu. Moyoni mwako, kama unaweza kuamini, itatendeka.

236 Unaamini hilo, bwana, unayeketi papo hapo na suti hiyo ya kijivu, unayeketi huko nyuma kabisa ukiniangalia? Unaamini hilo? Basi wasiwasi wako ulikuacha. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu. Hatufahamiani, sivyo, bwana? Hiyo ni kweli. Huo ndio unaougua nao.

237 Kusudi upate kujua, mimi nikiwa ni mtumishi wa Mungu, mwanamke aliyeketi karibu nawe anaugua ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli. Unaamini? Inua mkono wako, kwamba unaamini umeponywa. Kuwa tu na imani.

238 Mwanamke anayeketi karibu naye ana ugonjwa wa moyo. Unaamini hilo, ya kwamba Mungu atakuponya? Vema, bwana. Kama unaamini, unaweza kuupata.

239 Anayeketi karibu naye ana matatizo ya kike. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya?

240 Mwanamke anayeketi karibu na huyo, huyo mwanamke mnene, ana kisukari. Unaamini Mungu atakuponya?

241 Mwanamke anayeketi hapo juu ana shida fulani. Ana—ana matatizo ya kike, anayeketi hapo juu mwishoni mwa safu.

242 Ninaamini huyo ni binti yake anayeketi papo hapo nyuma yake pale, ana namna fulani ya ugonjwa wa kichwa, uliosababishwa na ajali. Hiyo ni kweli? Inua mikono yako, huko kwenye roshani.

243 Yeye ni nini? Mimi ni shahidi Wake, kwamba Yeye yu hai hapa alasiri ya leo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye huyatimiza Maneno Yake yote. “Kazi nizifanyazo mtazifanya.” Ni nani aliyewafanya hao watu, huko juu roshani? Mtu mwingine aamini, kwa dakika moja.

244 Sasa mnanitaka niwaonyeshe baadhi ya wasioamini? Huenda likawaaibisha. Ni wangapi wameona likifanywa? Hufanya tu. Huna budi kuacha ngano na magugu yakue pamoja.

245 Watu wote kwenye safu hii hapa, walio na kadi za maombi, fanyeni ninii . . . Ngojeni, hebu tutulie kwa dakika moja.

246 Ni wachungaji wangapi waaminio walioko hapa alasiri ya leo, walio ke—kesini, pia, nanyi mnaamini kwamba Marko 16 ni kweli? Inueni mikono yenu. Wachungaji wote waaminio waje hapa.

247 Kama nikiondoka hapa, na muone kile kitakachotukia alasiri ya leo, na watu hawa wakiponywa; halafu baadhi yao waseme . . . Mnaona, kwa kawaida, mwinjilisti mwenye huduma tofauti kidogo angeingia, anamwacha mchungaji baridi, mbele za kusanyiko. Kusanyiko linasema, “Loo, kama Ndugu Roberts akirudi, Ndugu Osborn, Ndugu *Nanii*, ama Ndugu Branham, mtu fulani, loo, yeye . . . ” Mchungaji wako ana haki ile ile kwa jambo

hili ninalofanya; mtu yeyote yule. Unaona, mchungaji wako ni mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, sawasawa na mwinjilisti mwingine yeyote.

248 Basi nataka wachungaji, wanaomcha Mungu kweli waje hapa na kusimama pamoja nami kwa dakika moja. Njoni huku kwa dakika moja tu, mfanye mistari miwili papa hapa. Ninamaanisha wale wanaoamini kweli sasa. Msiwaruhusu wasioamini kuja huku; mtawazuia wagonjwa. Kama—kama ukiamua Andiko hili ni kweli, na leo hii wakati Mungu ametutokea hapa na kuonyesha ya kwamba anafanyiwa mashtaka. Nasi tumemwamini na kujua ya kwamba anasema kweli na ni wa kweli. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, kama mnaamini! Amina.

249 Unaamini huo wasiwasi ulikuacha, bwana, unayeketi hapo mwishoni? Unaamini atakuponya? Vema.

250 Na ugonjwa wako wa tumbo, uliye karibu naye, je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya ugonjwa huo wa tumbo na kukupa afya? Unaamini hilo, unaweza kulipata pia.

251 Hawa ndio wachungaji waaminio pekee humu ndani leo? Vema, hao wanatosha. Mmoja anatosha.

252 Hebu watu wote walio na kadi za maombi, wanaoamini Marko 16 . . .

253 Sasa kumbukeni, usije kamwe endapo huamini. Unaona? Usije huku juu, katika unafiki huo. Unaona? Hilo ni baya kuliko kila kitu. Kama huliamini, sema, "La, siliamini," endelea na Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, ama mtu mwingine.

254 Lakini kama wewe ni Uzao halisi wa Ibrahimu, nawe unataka kuchukua msimamo wako. Uamuzi wako ume—umefanywa, na unataka kuuonyesha ulimwengu kwamba uamuzi wako umefanywa, kwamba unaamini kila Neno ambalo Yesu Kristo alisema ni sawa. Nao mashahidi walikuthibitishia, alasiri ya leo, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

255 Hebu wale walio na kadi za maombi *hapa*, washuke moja kwa moja hapa na kusimama papa hapa. Sasa simameni tu papo hapo, kama mtaweza. Sasa fanyeni tu mstari. Halafu wote walio katika sehemu hii *hapa*, walio na kadi za maombi, geukeni na mzunguke nyuma, kisha mwingie mstarini papa hapa nyuma yao upande huu. Sasa hebu wote walio—walio katika sehemu hii nyingine *hapa*, wageuke na kurudi ukutani, huko, na kufuatilia papa hapa nyuma ya mstari huu hapa, wanaposhuka. Hebu wote walio kwenye roshani wafuatilie moja kwa moja nyuma ya huu. Ninyi nyote mlio na kadi za maombi, mnaotaka kuombewa, na mmeamua, uamuzi wenu umetolewa, umefanywa na ukafikiwa, elekeeni kwenye ukuta na mfanye mstari mkija papa *hapa* nyuma.

256 Sasa, Biblia ilisema nini? Hebu niisome tena. Jambo la ajabu, ilifunguka tu kwenye mahali hapo. Ninaamini Bwana anataka tusome hayo tena, mnaona. "Baadaye akawatokea wale kumi na mmoja." Ametufanyia vile vile, alasiri ya leo. Yupo hapa. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Kristo na Roho Mtakatifu, ya kwamba Roho wa Kristo ni Roho Mtakatifu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, ndiye.

257 Hamna Miungu watatu wala wanne. Kuna Mungu mmoja tu. Kuna sifa tatu za Mungu; Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, bali si Miungu watatu. Huo ni ukafiri. Mnaona, kuna Mungu mmoja tu. Na hizo ni sifa. Mungu Baba alikuwa nyikani, kama Nguzo ya Moto. Vema. Mungu Mwana; Mungu Baba aliumba mwili ambao ulikuwa ni Mungu Mwana, kisha akaishi ndani ya Mwana. Mnaona? "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Iwapo wewe ni Mkristo, unaliamini. Halafu, basi, "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena." Basi sasa tazama, Yesu alisema, "Nalitoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu." Baada ya kufa Kwake, kuzikwa, kufufuka, alipaa juu.

258 Na wakati Sauli wa Tarso alipokuwa ameshika njia kwenda Dameski, Mwanga mkuu, Nguzo ya Moto tena, ilipiga mbele zake. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ilifanya nini? Ilimpiga kwa upofu. Ndipo alipoamka, alisema . . . Sasa kumbukeni, yeye ni Mwebrania. Alijua hiyo ilikuwa ni nini, la sivyo asingalisema, "Bwana." "Bwana, U Nani Wewe?" Alijua ya kwamba watu wake waliifuata Nuru hiyo, Nguzo hiyo ya Moto. Iliwatoa Misri. "Bwana, U nani Wewe ninayemuudhi?"

259 Akasema, "Mimi ni Yesu. Naam, ni vigumu kwako kupiga teke mchokoo."

260 Ni yeye aliyekuja kama Nguzo ya Moto usiku ule na kumtoa Petro gerezani.

261 Na sasa angalia, kama roho yuyo huyo akirudi, hivi hatakuwa na sifa zile zile alizokuwa nazo hapa, kama ni Nuru ile ile? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, Nguzo hii ya Moto ni nini, Ile? Sasa, kama kamwe sitawaona ninyi wanaume tena, nanyi watu, ushuhuda wangu umethibitika kuwa ni kweli. Biblia inaushuhudia.

262 Ulimwengu wa kisayansi unaushuhudia, yule, George J. Lacy alisema, "Mara nyingi nilisema ilikuwa ni saikolojia, mimi mwenyewe, Bw. Branham. Lakini," kasema, "nimeichunguza chini ya mwali usioonekana kwa jicho na kila namna ya mwali mkali mno na kila kitu ninachoweza kupata. Ile Nuru iliipiga lenzi, nayo lenzi hii haitapiga picha saikolojia."

263 Kwa hiyo niishi nife, ni kweli, kwa vyovyote vile. Kanisa linajua hilo, ni kweli. Sayansi inajua hilo, ni kweli. Sasa vipi kuhusu wewe? Kumbukeni, sio mimi. Ni Yeye. Sio mimi. Mimi

si kitu ila mmoja wenu tu ninyi nyote. Ni Yeye. Hana budi kumpata mtu fulani. Hakuna mtu anayestahili, bali mtu fulani hana budi kulifanya. Kumbukeni, sio kazi rahisi, bali ni kazi yenye utukufu kujua ya kwamba Bwana wako yupo hapa na unaweza kuwaambia ndugu zako Ukweli. Ila ni vigumu wakati hawataamini, bali, hilo, sote hatuna budi kukabiliana na hilo. Kumbukeni sasa.

264 Sasa, ninyi wasikilizaji, nyote mko karibu kupanga mstari sasa? Inaonekana kana kwamba wamepanga. Sasa kama kuna wengine kwenye roshani, fuatilieni moja kwa moja nyuma ya mstari huu hapa.

265 Sasa kumbukeni, hawa ni wachungaji wenu na kadhalika, watu wa Mungu, ambao wanamwamini Mungu. Hivi ninyi ni waaminio? Mlisimama hapa kufanya ushuhuda ya kwamba mnaamini hii Marko 16 ni kweli? [Wahudumu wanasema, "Amina."—Mh.] Vema.

266 Sasa Biblia ilisema, "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa; Mungu atamwinua. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa tutawaombeeni, sasa, wakati mmesimama kwa uchaji, kimya. Ndipo mtakapopitia hapa, sawa na mlivyokuwa mkija . . .

267 Mlikuwa mmekiri ya kwamba mnaamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Kisha mnaenda kwenye kidimbwi mkabatizwe, ama kijito, mto, ama popote pale. Ndipo mkibatizwa, hayo ndiyo tu mhubiri anayoweza kufanya. Kulihubiri Neno; mnaliamini; mnabatizwa kwa ondoleo la dhambi zenu; mnafufuka katika maisha mapya. Ndipo jinsi mnavyotenda, tangu hapo na kuendelea, inathibitisha kama kweli mlimkubali Kristo au la.

268 Sasa kama mnaamini katika Uponyaji wa Kiungu, na mmemkubali sasa kama mponyaji wenu, tumesimama hapa kuwawekea wagonjwa mikono. Jinsi unavyotenda, tangu mwisho wa mstari huo na kuendelea, maishani mwako mwote, yatakuwa ndiyo hakimu, haidhuru utasema nini. Mnaona ninalomaanisha? Nawe uko na hakika tu ya kupata afya kadiri ulivyo na hakika kudumu Mkristo. Utakuwa Mkristo kwa muda gani baada ya hapo? Mradi tu unaamini. Nawe umeponywa mradi tu unaamini.

> Angalieni*, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;*
>
> *Watashika nyoka;. . .wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono* yao *juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*

269 Katika kukabiliwa na hili, moyo wangu ulifikia uamuzi kadiri ya miaka thelathini na mitano iliyopita. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa kumwamini, Yeye amejitambulisha

hapa alasiri ya leo, thibitisho lisilokosea, mwujiza. Lolote lisiloelezeka ni mwujiza; kuonyesha, Yeye hufanya kila wakati.

Mnasema, "Mbona usininii tu . . ."

270 Hivi mlijua, mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Naye akasema, "Nimekuwa dhaifu." Ni wangapi wanaojua hilo? "Nguvu zimenitoka." Sasa, Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Mnaona?

271 Bali aliahidi lingefanya hivyo. Ni ahadi Yake. Haimbidi kulifanya, bali aliahidi angefanya.

272 Sasa je! mnaamini hilo, nyote kwenye mstari huu, mnaamini? Moyo wenu umeufikia uamuzi huo? Sasa itakuwa ni juu yenu sasa. Mioyo yenu imefikia uamuzi huo, ya kwamba mnaamini kwamba Yesu Kristo alisema Maneno haya. Kama mnaamini, ninyi kwenye mstari wa maombi inueni mikono yenu. Nyote kwenye mstari wa maombi, upokeeni uponyaji wenu juu ya msingi wa hili, kwamba mnaamini wachungaji wenu na sisi sote, ya kwamba tunamtumikia Mungu wa kweli aliye hai. Na ushahidi huo Wake mliouona alasiri ya leo, unamtambulisha hapa pamoja nasi, Yule aliyelifanya Neno, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama mnaamini, inueni mikono yenu. Halina budi kutukia, lazima litatukia tu! Sijali wewe ni nani, kama utadumu pamoja na hilo, halina budi kutukia. Kama tu vile mvua ijavyo; kama tu vile Musa alivyowatoa Misri; kama vile bikira alivyozaa mtoto pasipo baba wa duniani; litakuwa ni jambo lile lile, ikiwa hutalishuku.

273 Roy, njoo hapa sasa na kuichukua hii, tuimbe *Amini Tu*. Hebu kidogo, mpaka tutakapoomba. Wahudumu, na tuviinamishe vichwa vyetu; kusanyiko kila mahali.

274 Baba yetu wa Mbinguni, ma—majaribu ya muda huu! Tunashangaa, Bwana, kwamba ni wangapi kweli wanaoamini. Mbegu imekwisha kupandwa. Neno limesomwa. Kristo, Roho Mtakatifu, ameonekana mbele zetu na kuonyesha ule Uzima uliokuwamo katika Nuru hii, Naye alikuwa ni Nuru ya ulimwengu, Yeye ni Nuru sasa. Yeye ni ile Nuru kuu ya Milele, Naye ameonekana mbele zetu, alasiri ya leo, na kufanya vile tu alivyosema angefanya katika kizazi hiki. Neno limenenwa kikamilifu. Neno limetambulishwa kikamilifu. Nao watu, sasa, laiti wangeliamini tu kikamilifu kwa moyo wao wote. Tunawaombea, Baba. Ondoa kutokuamini kote . . .

275 Jalia mtu ambaye angeshuhudia dhidi Yako, alasiri ya leo, maskini mzee Kutokuamini, Mwenye Kushuku, na Kukosa Subira, jalia aondolewe mbali kutoka miongoni mwetu leo. Jalia aende kwenye giza la nje. Jalia atoke kwenye jengo hili; kusudi shahidi mkuu wa utetezi, Roho Mtakatifu, aweze kulihuisha kila Neno wanapopitia hapa. Lijalie. Jalia watoke hapa, mi—mioyo yao tayari imetoa uamuzi, nao wanapitia hapa.

276 Na sasa, ewe Roho Mtakatifu, wahuishie Neno hilo, kwamba kazi imekwisha mara utumishi wa mwisho umefanywa kwa kuwawekea wagonjwa mikono. Tujalie, Bwana. Ninadai kila moja ya uponyaji wao, katika Jina la Yesu Kristo.

277 Sasa, jambo lingine la kufanywa, ni kuwekea mikono. Kama tu sherehe ya ubatizo, nawe unazikwa pamoja Naye basi, kisha unafufuka na kuondoka ukiwa na maisha mapya. Mnaona? Huenda usijisikie hivyo, bali amini. Endelea tu kudumu nalo; hatimaye, baada ya kitambo kidogo, utakuta una maisha mapya. Hivyo ndivyo ilivyo hapa. Ni mbegu iliyopandwa. Tunapanda sasa, kwa kuiwekea mikono. Tunafanya nini katika hili? Kujitambulisha wenyewe. Kama vile katika Agano la Kale, waliweka mikono juu ya dhabihu zao, kujitambulisha wenyewe; kwa imani tunaiweka mikono yetu juu ya Kristo, kujitambulisha wenyewe na Yeye. Leo hii tunaweka mikono yetu juu ya wagonjwa, kujitambulisha wenyewe na Neno hili. Mnaona? Amini sasa, Naye Bwana atakupa afya.

278 Sasa, Ndugu Borders atakuwa akiimba, kwa utulivu, na vinanda, piano, na kadhalika, *Amini Tu*. "Mambo yote yanawezekana, amini tu."

279 Na hebu wazia tu sasa, Yesu akishuka kutoka kwa mlima ule. Hapo wanafunzi walikuwa wameshindwa, juu ya ugonjwa wa kifafa, akiwa amewapa nguvu kutoa pepo, siku chache tu kabla ya hapo. Si kwamba hawakuwa na nguvu, bali Yeye alisema, "Kutokuamini kwenu ndiko kulisababisha hilo." Mnaona? Bali alipokuja kwa Yesu, alijua ya kwamba aliigonga imani pale.

280 Sasa amini kwa moyo wako wote, sasa, wakati tukiimba kwa utulivu *Amini Tu* sasa. Ndugu Borders.

281 [Ndugu Branham na wahudumu wanaomba na kuweka mikono juu ya wale wanaopitia kwenye mstari wa maombi, huku kusanyiko linaomba na kuimba kwa utulivu *Amini Tu*. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> . . . amini,
> Mambo yote yawezekana, amini tu.

282 Sasa hebu tuuimbe namna hii, wote wanaoamini.

> Sasa naamini, (Mnaamini? Na tuinue mikono yetu!) sasa naamini,

283 Ee Mungu! Katika Jina la Yesu, waponye hawa, Bwana, ambao leso hizi zinawawakilisha. Kwa ajili ya utukufu Wako, lijalie, Bwana.

> . . . naamini;
> Sasa naamini, loo, sasa ndio naamini,
> Mambo yote yanawezekana, sasa ndio ninaamini.

284 Mnajua kile tumefanya? Tumezifuata amri za Yesu Kristo. Sasa ungali una uamuzi wako, "Nimeponywa. Haiwezekani

nisipate afya, kwa kuwa Mungu alitoa ahadi. Kwa midomo yangu inayokufa, jambo la mwisho midomoni mwangu, 'Ninaamini nimeponywa.'"? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaliamini hivyo? Ninaliamini. Mungu akubariki, ndugu yangu, dada.

285 Sasa na tusimame kwa miguu yetu, kwa muda mfupi tu. Sijui itakuwa lini; ninatumaini ni sasa hivi:

> Lakini hata twonane! hata twonane!
> Hata twonane. . . pa Yesu. (Yeye yupo uweponi mwetu sasa.)
> Hata twonane! hata twonane!
> Mungu awe nanyi hata twonane tena!

286 Na tuinamishe vichwa vyetu, tunapouvumisha. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Mungu Awe Nanyi.*—Mh.] Hata tutakapoonana!

287 Ee Mungu, jalia Neno Lako liwe taa sasa. Yale tumeona na kusikia na kusoma, na jalia lituongoze hadi miguuni Pako. Jalia daima tubaki hapo, tukiliamini Neno Lako, kila kitu ulichoahidi. Tujalie, Bwana.

> Hata twonane! hata twonane!
> Mungu awe nanyi hata twonane tena!

288 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa wakati ndugu yetu mpendwa sana, Ndugu Johnson, akichukua maombi ya kuondoka. Mungu akubariki, Ndugu Johnson.

*Kesi Ya Mahakamani* SWA64-0412
(A Court Trial)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 12 Aprili, 1964, katika National Guard Armory huko Birmingham, Alabama, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org